# Nipashe

Ijumaa Agosti 23, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581777

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


**ACT** yakosoa vikali karipio la Kamishna Polisi

UKURASA 4

**Ajali** ya basi, lori ilivyokatisha uhai watu wanne

UKURASA 4

**TMA**: Kutakuwa na uhaba wa mvua, kuweni na hadhari

UKURASA 5


TENA KINA KABUDI, LUKUVI... Kutoka turufu yake Rais kisiasa hadi uchumi rasilimaliwatu kazini


BUFE

Ndivyo kutokurasimisha biashara zao kunavyowaweka kando kimafanikio

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Dodoma kuwa shule ya kilimo, darasa likielimisha wakati wote

UKURASA 11



# Vijana kujirekodi video chafu janga

• **Ufuatiliaji** wa jeshi wabaini mambo ya kutisha... *Ukurasa 3*

UKURASA WA 2

## WAMCHANGIA FEDHA WAKILI MADELEKA KWENDA KORTINI KESI YA 'AFANDE'

## Mpango: Puuzeni dhana ya ukame Dodoma, mkoa huu una fursa tele

UKURASA 3




Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, wakati akitoa tamko la kukemea vitendo vya watu kutekwa na kuitaka Serikali kupeleka huduma za kijamii Ngorongoro. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Mbowe: Rais Samia aunde tume ichunguze watu kupotea, utekaji

UK. 2

**MICHEZO** RAIS SAMIA AZISHUSHIA NEEMA SIMBA, YANGA UK.24

**MAONI,** UK.6

# Mbowe: Tume ichunguze watu kupotea, kutekwa

**Na Romana Mallya**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe amemwomba Rais Samia Suluhu Hassan, kutumia mamlaka yake kwa mujibu wa Sheria ya Uchunguzi Mahsusi ya Mwaka 2019, kuunda Tume ya Kimahakama ya Majaji kuchunguza tuhuma zote za watu kupotea, kuteswa na kutekwa.

Mbowe alitoa hoja hiyo jana mkoani Dar es Salaam wakati anazungumza na waandishi wa habari kuhusu mambo mawili aliyoyataja kuzua taharuki na hofu ndani ya nchi, yakiwamo madai ya baadhi ya viongozi wao na Watanzania kuendelea kutekwa na vyombo vya dola.

Jambo lingine alilolizungumzia ni kinachoendelea katika Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), baada ya maandamano ya baadhi ya wakazi waliomo katika eneo hilo wanaopinga kufutwa kwa vijiji vilivyomo ndani ya hifadhi hiyo.

Kuhusu utekaji, Mbowe alivishutumu vyombo vya usalama kuwa vimekuwa vinateka watu katika taratibu ambazo si za kisheria; kwa maana kutowafikishwa mahakamani na baadhi wakidaiwa kuwa wameuawa.

"Hili jambo linatakiwa likomeshwe na lisimamishwe kwa sababu sisi si malaika, yawezekana tuna makosa, tukamatane na tujitetee kwa utaratibu wa katiba ya nchi, siyo kututeka, kututesa, kutulazimishia tukubali makosa ambayo hatuna," alidai.

Mbowe alidai kuwa jeshi ambalo linatuhumiwa ndilo hilo linalojichunguza na kueleza kwamba "hawatakaa wapate ukweli".

"Tunamwomba Rais Samia atumie mamlaka yake kwa mujibu wa Sheria ya Uchunguzi Mahsusi ya Mwaka 2019, kuunda Tume ya Kimahakama ya Majaji kuchunguza tuhuma zote.

"(Tume) iwasikilize waathirika, mashuhuda, ifuatilie mamia waliouawa katika utaratibu ulio tofauti. Rais ana mamlaka hayo. Na kwa sheria hii, (tume) haiwezi kuundwa na mtu yeyote isipokuwa Amir Jeshi Mkuu wa Nchi yetu.

"Kuliachia Jeshi la Polisi kukuletea taarifa eti "iko hivi, wanajiteka wenyewe", hii ni huzuni. Ichunguze haya anayoelewa Mbowe na mengine mengi ambayo hajayazungumza," alisema.

Mbowe alisema anaamini kwamba tume hiyo itakayoundwa itasimamia kweli na haki na kurejeshea watu uhuru wao kwa wale wanaoshikiliwa katika njia ambazo si za utaratibu wa kawaida.

Pia alimwomba Rais Samia kupiga marufuku kitu kinachoitwa 'Task Force' ya vyombo vya ulinzi na usalama kwa madai kuwa havifuati sheria, bali utashi wa watu binafsi.

Mbowe alitolea mfano baadhi ya matukio yaliyotokea hivi karibuni, likiwamo linalohusisha viongozi wawili wa chama hicho wilayani Temeke na raia mmoja, ambao mpaka wakati anazungumza walikuwa hawajulikani waliko.

Alitaja watu hao ni Katibu wa Jimbo la Temeke, Jacob Mlay, Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la CHADEMA (BAVICHA), Wilaya ya Temeke, Desdedith Soka na Dereva Bodaboda, Frank Mbise.

Katika mkutano huo, Mbowe alitambulisha baadhi ya wananchi kwa madai wamepotelewa na ndugu zao kwa kutekwa, huku akitaja majina, namba na eneo la kazi la baadhi ya aliowaita askari wanaotekeleza vitendo hivyo.

"Askari hawa ninaowataja (majina yamehifadhiwa) wengine wamehusika katika mambo ya kihalifu na kitapeli kwa kutumia mwamvuli wa Jeshi la Polisi, haya mambo yafanyiwe uchunguzi, wanaohusika wanajua Mbowe ninasema kweli.

"Rais Samia afikirie tena, Julai 14, 2013, ilipitishwa bungeni Sheria ya Usalama wa Taifa. Sheria hii katika kifungu 4(3) kinatoa haki ya maofisa wa Usalama wa Taifa kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi, kukamata watu wanaowadhania wao wanahatarisha usalama wa nchi," alisema.

Mbowe alisema Usalama wa Taifa katika nchi, hawana mfumo ulio rasmi wa kukamata, kuhifadhi, kushtaki kama ilivyokuwa polisi kupitia P.G.O (Police General Orders), akimaanisha Kanuni za Jeshi la Polisi.

"Ndio sababu watu wakipotelewa na watu wao, wanakimbilia polisi ambako wanajua ndiko utaratibu wa kisheria, kumbe kuna mamlaka nyingine ya usalama inakamata watu na hajui wanawapeleka mahabusu ipi au kuwashtaki na nini.

"Tunamwomba Rais afute kifungu hiki, kukamata raia bila kutoa maelezo popote, bila kupeleka vituo vya polisi, bila raia kujua wanapelekwa wapi au raia kujua ndugu zao wanapelekwa wapi.

"Nimemwomba Rais kwa sababu leo mamlaka zote za vyombo vya ulinzi na usalama, kwa mujibu wa sheria hiyo, imerejeshwa katika mamlaka ya Rais," alisema.

Mwanzoni mwa mwezi huu, Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kilimshauri Rais Samia kuunda



tume maalum ya kuchunguza matukio yote ya kudaiwa kupotea kwa watu, kutekwa na kuteswa.

Pia alishauri Rais Samia kuunda tume maalum ya kuchunguza ushiriki wa Jeshi la Polisi katika masuala ya utekaji kwa wanachodai kuwa jeshi hilo limekuwa linatuhumiwa kushiriki katika vitendo hivyo.

Julai 15 mwaka huu, Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Camillus Wambura alisema Jeshi la Polisi halihusiki na matukio yanayodaiwa kuwa ni ya utekaji, kwa kuwa jukumu la msingi na la kikatiba la jeshi hilo ni kuhakikisha linalinda usalama wa raia na mali zao.

IGP Wambura alitoa kauli hiyo akiwa mkoani Simiyu katika ziara yake ya kuzungumza na maofisa, wakaguzi na askari wa vyeo mbalimbali.

**NGORONGORO**

Kuhusu kinachoendelea Ngorongoro, Mbowe alisema CHADEMA inaungana na wale wanaosema Wamasai walioko katika Hifadhi ya Ngorongoro ni raia halali wa Tanzania, wenye maeneo yao ya asili, yanayopaswa kuheshimiwa na kuenziwa pamoja na utajiri mkubwa wa wanyamapori unaozunguka maeneo hayo.

"Bila kujali nani amesimama wapi, tatizo la Ngorongoro haliwezi kumalizwa kwa mtutu ya bunduki, ndio msimamo wa CHADEMA.

"Serikali irudi katika meza ya kuzungumza na wananchi wahamishwe kwa ridhaa na ushawishi wataopewa na si kutumia vyombo vya ulinzi na usalama," alishauri.

Mbowe pia alizitaka mamlaka za uchaguzi zirejeshe haraka haki ya wananchi hao kushiriki michakato yote ya kuchagua na kuchaguliwa.

Agosti 18 mwaka huu, NCAA kupitia taarifa yake kwa umma, ilisema hakuna ukiukwaji wa haki za binadamu na shughuli za utalii katika eneo la hifadhi hiyo zinaendelea kama kawaida.

MARCAS DEBT COLLECTORS & AUCTIONEERS (T) LTD.

**TANGAZO LA MNADA**

MARCAS DEBT COLLECTORS AND AUCTIONEERS LTD, kwa idhini iliyopewa na **State Grid Electrical and Technical Works Limited** tutauza Transfoma kwa njia ya mnada. Mnada utafanyika siku ya 14 baada ya tangazo hili.



**Masharti ya Mnada**
1. Mshindi atalipa asilimia 25% papo hapo au hela zote papo hapo baada ya nyundo ya dalali kushuka. kiasi kinachobakia , yaani asilimia 75% italipwa ndani ya siku 14 (kumi na nne)baada ya siku ya mnada. atakayeshindwa kulipa hizo asilimia 75% katika muda huo, ushindi wake utafutwa na hautarudishiwa kiasi ulichotanguliza. Mali hiyo itanadishwa tena.
2. Transfoma ni jipya litauzwa jinsi lilivyo na linafanya kazi 800kVA 11/0.4kV.
3. Siyo lazma mwenye kutoa bei ya juu ashinde. Mnadishaji ana haki ya kuamua kutokana na bei ya hifadhi kama ilivyoagizwa na mfilisi.
4. Gharama zote pamoja na usafiri, malazi, ukaguzi na kuhamisha umiliki wa mali ni juu ya mnunuzi mwenyewe

**Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na:**
**Marcas Debt Collectors and Auctioneers Limited**
**Safari Hotel Building, 2nd Floor,**
**P. O. Box 16823, ARUSHA.**
**Simu Na. 0787151550 au 0713268383**

## Wamchangia Wakili Madeleka kwenda kortini kesi ya 'Afande'

**Na Jenifer Gilla**

BAADHI ya watu wamejitolea kumchangia fedha Wakili Peter Madeleka na wenzake kusikiliza kesi dhidi ya Mrakibu Msaidizi wa Polisi (ASP), Fatma Kigondo, wanayemtuhumu kutuma vijana kubaka na kulawiti binti anayedaiwa mkazi wa Yombo Dovya, wilayani Temeke, mkoani Dar es Salaam.

Kesi hiyo ilifunguliwa Agosti 20 mwaka huu na Wakili Paul Kisambo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma na kupewa namba 0000058901 kwa tuhuma za kumfanyia ukatili wa kijinsia binti huyo na video yake kusambazwa kwenye mitandao kijamii.

Kupitia ukurasa wake wa X, Wakili Madeleka aliarifu umma kuwa kesi hiyo inatarajiwa kusikilizwa leo na kuwaomba Watanzania wachangie gharama za usafiri wa mawakili watakwenda kusimamia kesi hiyo kwa upande unaoshtaki.

Saa moja baadaye, Wakili Madeleka aliweka ujumbe kuwa kuna uwezekano mkubwa atashindwa kusafiri kwenda Dodoma kwa ajili ya kusikiliza kesi hiyo kutokana na kukosa fedha.

"Kwa sababu ya kukosa fedha, kuna uwezekano mkubwa kesho nitashindwa kwenda Dodoma kwa ajili ya kesi ya jinai inayomkabili ASP Fatma Kingondo, ngoja tuendelee kumwachia Mungu," aliandika.

Ujumbe huo uliamsha hisia za watu waliomtaka aweke namba ya kuchangia fedha na wale waliokamilisha miamala waliweka risiti kwenye ukurasa wa wakili huo kuthibitisha kuwa wametoa mchango wao.

Tukio hilo liliibuliwa na aliyekuwa Meya wa Ubungo, Boniface Jacob wiki mbili zilizopita ambaye aliandika mkasa mzima kwenye ukurasa wake wa X huku akiwatumia nakala Rais Samia Suluhu Hassan, Waziri wa Ulinzi, Dk. Stergomena Tax na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dorothy Gwajima.

Baada ya kusambaa kwa taarifa za tukio hilo, Jeshi la Polisi lilikamata vijana wanaodaiwa kutekeleza ukatili huo na kuwapandisha mahakamani, lakini kukawa na shinikizo 'Afande' anayetuhumiwa kutuma vijana hao, naye afikishwe kortini.

Mawakili waliojitia "wa haki", akiwamo Madeleka waliamua kumshtaki ofisa huyo wa polisi, wakimhusisha na ukatili huo.

# Mpango: Puuzeni dhana ya ukame Dodoma, mkoa huu una fursa tele

**Na Joyce Lameck**

MAKAMU wa Rais Dk. Philip Mpango, amewataka wananchi wa Mkoa wa Dodoma kuondoa dhana ya kuamini mkoa huo hauna fursa kutokana na ukame, badala yake wazitambue fursa zilizopo.

Aidha, alizitaja fursa zilizopo kwenye kilimo, ufugaji, utalii wa asili na uchimbaji wa madini.

Akihitimisha ziara ya siku nne mkoani humo, alisema ni muhimu wananchi wakaziona fursa hizo ambazo haziwezi kupatikana maeneo mengine nchini.

Pia, aliwataka kutunza mazingira kwa kutokata miti ovyo na ili kuweka mazingira ya kijani katika mkoa huo, kwa ajili ya kutimiza mpango wa kutumia nishati safi ya kupikia kwa Watanzania ifikapo mwaka 2030.

"Nafikiri tulilishwa matango pori, mnayajua? Kuwa tuliambiwa Dodoma ni nusu jangwa si ndiyo, kwakweli hilo ni tangopori fursa zipo nyingi, hata nikasema ni kiasi cha mvua inayonyesha ni kwamba hatuyatengi yale maji kuyatumia wakati mwingine.

"Lakini tuna bahati sana watu wa Dodoma akatuwekea maji mengi sana chini ya ardhi, halafu tukaambiwa hivyo na sisi tukakubali tukalala usingizi Dodoma ina fursa nyingi," alisema Dk. Mpango.

Alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa mapinduzi katika kilimo, kwa kuwa kutokana na kilimo cha umwagiliaji kumekuwa na mafanikio ya ukuaji wa sekta hiyo kwa asilimia 10 ifikapo 2030.

Dk. Mpango aliagiza utekelezaji wa mradi wa BBT Chinangali, kuwa wafugaji wapewe eneo ambalo litaruhusu kuendeleza shughuli za ufugaji, waandaliwe BBT ya wafugaji, na kwamba uambatane na ujezi wa kituo cha afya.

Vilevile, alikubaliana na ombi la kuwapo kwa barabara ya lami kutoka Mpunguzi kuelekea katika mradi huo, kuwa jukumu hilo libebwe na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD) ili kusaidia Wakala wa Barabara Vijijini (TARURA) kutokana na urefu wa barabara hiyo yenye kilomita 100, pia itakuwa ni njia ya kwenda kufanya utalii Hifadhi ya Taifa Ruaha (RUNAPA).

Awali, Mkuu wa Mkoa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema kuwa pamoja na maendeleo yanayofanywa na serikali katika maeneo ya mjini, lakini pia Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa ni Rais anayejali hata watu wa hali ya chini kwa kufungua miradi mbalimbali katika mkoa huo.

Waziri wa Madini na Mbunge wa Dodoma Mjini, Antony Mavunde, alisema wizara yake itahakikisha inawajibika kusimamia wananchi wa mkoa huo wana nufaika na rasilimali ya madini amabayo Mwenyezi Mungu amewajalia.

Aidha, wizara imeshaanza kufanya utaratibu wa kutembelea maeneo yote ya uchimbaji ili kwenda kujirithisha na usalama wa maeneo ya uchimbaji, pia utaratibu wa sheria pamoja na mazingira kuwa inafanywa kwa sheria inavyoelekeza.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Festo Dugange, aliagiza kufanyika kwa tathmini ya mfuko wa ujezi wa hospitali ya Mloa, njia kutoka wodi moja kwenda nyingine kama kuna upungufu wa fedha ielezwe.

"Taarifa ifikishwe katika ofisi yao ili kutolewa fedha hizo kwa haraka, kukamilisha ujezi wa njia hizo kwa haraka kwani hospitali ni muhimu kuwa na njia hizo," alisema.

Alisema serikali imenunua magari matano kati yake manne ni maalum kwa ajili ya wagonjwa na jingine usimamizi wa huduma za afya katika majimbo mawili ya Mvumi na Chamwino.

Naye Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, alisema Tanzania imetoka mbali kwenye kilimo na kuwa dira ya sasa ndiyo itakayo badilisha maisha ya Mtanzania mmoja mmoja kwenye kilimo kwa kutosubiri msimu wa kilimo katika mwaka.

Aidha, alisema mradi wa BBT Chinangali unakwenda kunufaisha wakulima wengi katika mkoa wa huo, kwa kuwa ni mkubwa pamoja na mabwawa ambayo tayari yameshakamilika, lakini bado inaendelea kutekeleza miradi mingine ambayo itaweza kusaidia katika kilimo cha umwagiliaji.

Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Kundo Matthew, alisema changamoto ni sehemu ya maendeleo, hivyo wanaamini yataendelea kutokea kwa kuwa wananchi wanapoendelea kutoa mahitaji yao kuhusu maji, wizara iendelee kutekeleza majukumu yake.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Umwagiliaji, Raymond Mndolwa kuhusu Mradi wa Jenga Kesho Iliyobora (BBT) wa Skimu ya Umwagiliaji ya Dk. Samia Suluhu Hassan Mlazo/Ndogowe, alipowasili kwa ajili ya kuweka jiwe la msingi la mradi huo, Kijiji cha Mlazo, Wilaya ya Chamwino akiwa ziarani mkoani Dodoma jana. **PICHA: OMR**

# Matukio vijana kujirekodi picha chafu yaongezeka

**Na Salome Kitomari**

DAWATI la Jinsia na Watoto Mkoa wa Kipolisi Ilala limebaini matukio ya vijana kujichua, kujirekodi picha za utupu na kurusha mtandaoni yameongezeka, jambo ambalo ni ukatili na hatari kwa afya.

Kutokana na hali hiyo, dawati hilo limekuja na kampeni ya 'Tuwaambie Kabla Hawajaharibiwa' kwa shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu.

Akizungumza wakati wa mafunzo kwa askari wa dawati la jinsia na watoto mkoani humo jana, Mratibu wa Mafunzo hayo, Dk. Christina Onyango, alisema wanafanya mafunzo hayo ili askari wawe na uelewa wa pamoja kuhusu kampeni hiyo na watafundishwa kuhusu ukatili, rushwa ya ngono na maadili.

"Kesi za ukatili mtandaoni zipo, vijana wengi wanafanya mapenzi wanajirekodi, baada ya kujirekodi wakiwa wanafanya mapenzi wanapogombana mmojawapo anachukua video anarusha kwenye mtandao. Tumejitahidi sana kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kudhibiti, lakini bado yapo," alisema.

"Kuna ukatili ambao watoto wetu wanaufanya sana ni ukatili wa kujichua. Wao hawajui kwamba wanajifanyia ukatili. Niliwahi kwenda kwenye chuo fulani kufundisha nikawa nawaeleza athari za kujichua, alitokea mwanafunzi mmoja akasema:

"Mimi nilikuwa sijui kwamba ni mbaya kwa kuwa wakati ninasoma tuliambiwa ukiwa na hamu unajichua, basi tulikuwa tunapanga mstari kisha tunajichua. Hawajui ni ukatili na baada ya kuwapa elimu waligundua kuna madhara kiafya na uzazi," alisema na kuongeza:

"Kutokana na mambo kama haya watoto wanajiingiza kwenye mapenzi ya jinsia moja si kwa wakike na kiume. Wazazi tuongee na watoto wetu wanapokuwa wamefika kuwa vijana, mabinti."

Dk. Christina alisema kesi ya matukio ya ubakaji na ulawiti zinaongezeka na wananchi wamekuwa na mwamko wa kuripoti matukio hayo, hatua zinachukuliwa kuhakikisha haki inapatikana.

"Tumeona tumekuja na kampeni hii ili kupunguza, tunasema tuwajengee uwezo kuliko kupokea wahanga, wajitambue na kujidhibiti mapema," alisema.

Akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto, Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Leah Mbunda, alisema kampeni hiyo inafanyika nchi nzima kwa kuwafikia wanafunzi wa shule za msingi na vyuo ili kung'amua ukatili.

"Tunalenga kuitoa kwa wanafunzi wanaoanza shule ya msingi na vyuo, tumewalenga hawa kwasababu wanatoka kwenye maeneo tofauti waliyoyazoea, huku wengine hasa wa vyuo wakitoka mkoa mmoja kwenda kwingine," alisema.

Alisema katika kufuatilia walibaini wanafunzi wanapokwenda maeneo mageni wanakuwa wageni wa mazingira, marafiki na masomo, hawajui mengi na kuangukia kwenye masuala ya jinai kwa kutenda au kutendewa kwa kujua au kutokujua.

"Mfano Dar es Salaam kuna vyuo vingi, tunapokea wanafunzi kutoka mikoa tofauti, lakini kuna aina tofauti za makosa. Makosa yanayowaandama ni kutapeliwa, mtu ametoka kwenye familia ya waaminifu wanao mwamini mtu yeyote anakuja Dar es Salaam anakutana na matapeli wanaotumia uaminifu.

"Lakini wanaweza kuja kwingine wakakutana na tamaa, anakotoka vitu havipo, hili la tamaa linawaingiza wengi kwenye unyanyasaji wa kingono, anakuja kuna mambo mengi hakuyaona kijijini alikotoka kisha anaingia kwenye vitendo vinavyomsababishia kufanyiwa ukatili.

Kamishna Leah alisema wengine wanafanyiwa ukatili kwa sababu wanataka fedha na mwishowe huingia kwenye matendo ya kiovu na lengo la kuja kusoma kutotimia, na kwamba wameona ni vyema wakawapata mapema na kuwapa taarifa muhimu ili wajiepushe.

"Kampeni hii tutakwenda kwenye shule na vyuo kwa kushirikiana na uongozi kwa kuwa kuna watu wa madawati na shule za msingi kuna mabaraza na walimu, tutatembelea shule zote ili kutoa elimu ya kina. Tutawafundisha na kuwaasa. Tunaamini itatusaidia kupunguza au kuondoa makosa yanayosababishwa na ugeni wa wanafunzi wanapokuja shuleni au vyuoni.

Aidha, aliwataka wanajamii kubeba jukumu la malezi kwamba wanapomwona mtoto yupo kituoni au eneo ambalo anaweza kufanyiwa ukatili azungumze naye kwa kuwa itamsaidia.

Aidha, alisema kampeni hiyo haijaja kuvunja kampeni nyingine kwa kuwa zitaendelea kama kawaida ili zote zisaidiane kupunguza na kumaliza ukatili kwenye jamii.

"Elimu ya malezi, elimu ya kutofanya ukatili kwa watoto, kampeni ya ukatili wa jinsia na watoto bado zinaendelea. Hii ni kampeni yetu sote watoto ni wetu, vijana ni wetu Maisha yanaanzia kwenye familia wote tuwajibike, tuisikilieze kampeni hii na tuitekeleze. Mtoto akitoka nyumbani akaenda shuleni tunasema yuko mikono salama ya walimu, lakini akitoka huko anarudi nyumbani ambako anakuwa kwenye mikono ya jamii anapotembea.

"Unapomuona mtoto ana sare za shule saa 12 jioni anazubaa zubaa zungumza naye, utakuwa umemwokoa sana huyu mtoto licha ya kwamba sio wa kwako kwasababu hatujui angekutana na mazingira gani hatarishi kwake," alisema Kamishna Leah.

Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto mkoa wa Kipolisi Ilala, Glory Urassa, alisema kampeni hiyo ni muhimu kwa kuwa itakwenda kusaidia watoto kujua mambo mengi muhimu kwa maisha yao.

Mafunzo hayo yamekutanisha askari wa vyeo vya chini, na leo ni wakaguzi na maofisa kutoka madawati ya kijinsia mkoani humo.




Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Wizara ya Nishati, Neema Mbuja (kushoto) na Meneja wa kampuni ya Burn Manufacturing ambao ni wadau wa nishati safi ya kupikia, Benson Mgaya, wakitoa elimu ya matumizi ya nishati safi kwa wananchi waliotembelea maonesho, wakati wa Tamasha la Kizimkazi linaloendelea visiwani Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ajali ya basi, lori yaua wanne

**Na Julieth Mkireri,**
CHALINZE

WATU wanne wamefariki dunia na wengine kujeruhiwa baada ya basi la kampuni ya Baraka kugongana uso kwa uso na lori.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Kamishna Msaidizi Pius Lutumo alisema jana kuwa ajali hiyo ilitokea jana saa 8:30 mchana katika eneo la Vigwaza, Chalinze, mkoani Pwani.

Alisema ajali hiyo ilitokea baada ya basi la abiria lililokuwa linatoka Dodoma, kutaka kuyapita magari mengine bila kuchukua tahadhari na hivyo kukutana uso kwa uso na lori lililokuwa linatoka Dar es Salaam kwenda Rwanda.

Kamanda Lutumo alisema waliofariki dunia kutokana na ajali hiyo ni wanawake wanne. Kati yao, yumo mtoto mdogo na maiti zao zimehifadhiwa Hospitali ya Chalinze huku majeruhi wakikimbizwa katika Kituo cha Afya Mlandizi kwa matibabu.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge alitembelea eneo la ajali na kueleza kuwa anasikitishwa na ajali nyingi zinazoendelea kutokea huku sababu ikichangiwa na baadhi ya madereva kutozingatia Sheria za Usalama Barabarani.

Aliomba wananchi kuwa wavumilivu na foleni zitakazokuwapo kwenye eneo hilo wakati jitihada zikiendelea kuhamisha mafuta kwenye lori lililopata ajali.

# ACT-Wazalendo yakosoa karipio Kamishna wa Polisi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Othman Masoud Othman, amesema chama chake kimepokea kwa uzito kauli ya karipio kwa wanasiasa iliyotolewa na Kamishna wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, mbele ya waandishi wa habari.

Kamishna huyo alizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni akiwaonya wanasiasa kuacha kejeli, matusi wanapokuwa kwenye majukwaa ya kisiasa kwa kufanya hivyo wanahatarisha amani ya nchi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika katika ofisi za chama hicho Vuga mjini Zanzibar, alisema nafasi ya polisi ni kulinda amani ya nchi na kusema kauli hiyo ina athari kwa nchi kuelekea uchaguzi mkuu 2025.

Kwa mujibu wa Othman, wananchi wanakuwa na wasiwasi na kauli yake kuelekea uchaguzi mkuu katika kulinda mustakabali wa nchi.

Alisema chama cha ACT kimetafakari taarifa hiyo na kuitolea ufafanuzi kuwa, imelenga upande mmoja pekee wa chama cha siasa.

Akifafanua, alisema alitegemea chombo hicho ni kielelezo cha uadilifu na haki katika kazi na matamshi yake yasingeegemea upande mmoja wa Chama cha ACT-Wazalendo.

Aidha, alisema kwa mtu mwadilifu anaweza kujiuliza Kamishna hakuyasikia matusi ya nguoni yaliyotolewa na viongozi wa CCM Agosti 10 kwenye Uwanja wa Amani Unguja dhidi ya viongozi wakuu wa ACT.

"Kwa mtu yeyote anayemwelewa Kamishna Hamadi kwa uweledi wake ni wazi taarifa yake ni shinikizo kutoka kwa viongozi wa vyama vya kisiasa na jambo hilo ndilo linaloleta maafa makubwa na kuharibu amani ya nchi," alisema Othman ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais.

Alisema matukio ya Zanzibar ya hivi karibuni ya uvunjifu wa amani ikiwamo matokeo ya kikatili na uvunjifu hajasikia Jeshi la Polisi kuchukua hatua dhidi ya matukio hayo.

Alisema Jeshi la Polisi linatambua jinai haina kikomo na wala haifi na kutoa mfano wa watu 21 kuuawa kikatili katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 akidai hakuna uchunguzi uliofanyika.

Aidha, alihoji Jeshi la Polisi linatoa wapi ujasiri kwa kusema wao ni walinzi wa amani ya nchi.

Othman alisema matokeo hayo jeshi hilo halioneshi kushtushwa na matukio hayo na badala yake wanashtushwa na kauli za viongozi wa ACT-Wazalendo.

Alitoa hadhari ya mustakbali wa kuelekea uchaguzi mkuu na amani na usalama ni dhamana ya watu wote, iwapo kila mmoja atatimiza wajibu wake kwa uadilifu na dhamira ya kweli amani itapatikana bila ya kutumia gharama ya fedha.

Kadhalika, alisema ujenzi huo una misingi yake na haiwezi kujengwa kwa usanii, makaripio wala matumizi ya nguvu.

Alisema haijawahi kutokea duniani matumizi ya nguvu kuwavunja moyo wananchi katika kudai haki yao ya kidemokrasia.

Hata hivyo, alisema hali ngumu ya maisha, ukosefu wa ajira na ufisadi kwa kiwango cha kutisha Zanzibar umesababisha watu wengi kuwa na hasira na kukata tamaa na kwamba vyombo vya ulinzi vinapaswa kufahamu hilo kwa mustakbali wa amani ya nchi.

"Juhudi za kuinusuru nchi yetu inaelekea kufika ukingoni kutokana na mbinu na ghiba za watawala," alisema.

Alisema kuelekea 2025 hakutakuwa na tofauti yoyote na chaguzi zilizopita na pengine hali itakua mbaya zaidi Zanzibar na kusababisha maafa.

Alimtaka Rais Samia aharakishe utekelezaji wa ripoti ya haki za jinai ili jeshi la polisi lifanyiwe mageuzi yanayostahiki kabla ya uchaguzi ujao.

"Jeshi liache kuegemea upande mmoja na badala ya kuleta amani na mtengamano unaleta taharuki na vitisho visivyo na sababu," alisema.

Alisema ACT-Wazalendo kitaendelea kusimamia wajibu wake wa kikariba kwa kufuata misingi na Mikoa ya Chaka ya kuisimamia serikali, na kwamba ni wajibu CCM kujibu hoja badala ya kulitegemea jeshi kufanya kazi hiyo.

Alisema jeshi hilo linapaswa kuchukua hatua dhidi ya matukio yote ya uhalifu na ukatili ili kupeleka ujumbe kuwa matokeo kama hayo hayatofanyika tena na Zanzibar inaweza kuendesha siasa na kufanya uchaguzi bila ya watu kuhujumiwa na kuuliwa.

Alisema njia pekee ya kuinusuru Zanzibar na machafuko ni kuendeshwa kwa haki na kusisitiza kuharakisha kutekeleza makubaliano kati ya Maalim Seif na Dk. Hussein Mwinyi ili kuiweka Zanzibar katika mustakbali mwema.

Kadhalika Chama cha ACT kitaendelea kuhubiri haki na kuwahimiza wananchi kupambania haki yao pale itakapoporwa. Pia, kitaendelea na utaratibu wake wa kusimamia serikali kwa sababu huo ni wajibu wao na CCM wajibu wao wajibu hoja na wasitegemee jeshi la polisi kuwajibika.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

## UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA MWANZA NA SHINYANGA

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza mzunguko wa tatu unaanza kufanyika tarehe 21 hadi 27, Agosti, 2024 katika Mikoa ya Mwanza na Shinyanga kwa siku saba kwa kila kituo.

1. **SIKU:** Uboreshaji unaanza siku ya Jumatano tarehe 21 na kuhitimishwa Jumanne tarehe 27 Agosti, 2024.
2. **VITUO:** Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 9 na kubonyeza.Kisha atachagua Namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

***KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA***

**Limetolewa tarehe 16 Agosti, 2024 na:**

**Kalima, R. K.**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

## Tanzania yashinda medali nne mashindano ya hisabati Afrika

Na Mwandishi Wetu

TANZANIA imeshinda medali nne za shaba kwenye mashindano ya nchi za Afrika ya Hisabati yaliyofanyika Chuo Kikuu cha Witwatersrand, Afrika Kusini, Agosti 13 hadi 20, mwaka huu kwa kuhusisha zaidi ya nchi 25 barani Afrika.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa Chama cha Hisabati Tanzania (CHAHITA), Dk. Said Sima, alisema kwa mara ya kwanza Tanzania imefanikiwa kupata medali nne za shaba ambazo kwa miaka mingi haikuwahi kuzipata.

Alisema mashindano hayo yametoa hamasa kwa wanafunzi kupenda somo la hisabati na kudhihirisha kuwa wanahisabati wa Tanzania wanaweza kushindana na nchi nyingine.

Aidha, alitoa wito kwa wanafunzi kuongeza juhudi na kuondoa uoga wa kudhani kuwa somo la Hisabati ni gumu kutokana na mitazamo mbalimbali iliyopo kwenye jamii.

Wakizungumza baada ya kuwasili kutoka Afrika Kusini wanafunzi walioshiriki kwenye mashindano hayo wamesema kilichowasaidia kushinda ni bidii, masomo ya ziada ya maandalizi pamoja na kutokata tamaa.

Washiriki hao walishukuru ushirikiano walioupata huku wakiwaasa vijana hasa wanawake kujitokeza kushiriki kwenye mashindano hayo.

Washiriki watano walidhaminiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Dk. Philip Filikunjombe, alisema hatua hiyo ni sehemu ya juhudi za mamlaka hiyo kuchochea ukuaji wa masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabari (STEM) nchini.

Alisema lengo jingine ni kuendeleza stadi za teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) miongoni mwa wanafunzi.

Mkurugenzi huyo alisema TCRA itagharamia elimu kwa wanafunzi walioshiriki kwenye mashindano hayo, ambao majina yao na shule za sekondari kwenye mabano ni Zakaria Mataiga Mwita (Iloboru High School Kidato cha 4 (PCM), na Stella Ludan Maliti Marian Girls High Scool Kitato cha 4 (PCM).

Aidha, aliwataka wanafunzi na wanazuoni wa Tanzania kupenda masomo ya STEM (Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hesabu) yanayojenga misingi imara ya umahiri na ubunifu kwenye TEHAMA teknolojia imekuwa kwa kasi na hivi sasa kuna Akili Mnemba (AI) na programu tumizi nyingi zinazowezesha shughuli nyingi.

Wanafunzi walioshiriki mashindano hayo ni Amborse George Rutashobya wa Shule ya Sekondari ya Ufundi Iyunga; Ilham Abdalla Awadhi wa Feza, Zanzibar; Mwanaarab Said Mbwana wa Sekondari ya Lumumba, Zanzibar; Stella Ludan Maliti wa Sekondari ya Wasichana ya Marian na Zakaria Mataiga Mwita wa Azania.

# Mikoa 15 kukumbwa uhaba wa mvua za vuli, joto kali

Na Faustine Feliciane

MIKOA 15 inatarajiwa kuwa na uhaba wa mvua za vuli ambao utaleta athari kwenye sekta mbalimbali na kuwapo kwa ongezeko la joto kwa mujibu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

TMA jana kupitia kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Dk. Ladislaus Chang'a, imetoa utabiri wa mvua hizo ambazo zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Septemba.

Dk Chang'a, alisema kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa katika kipindi chote cha msimu kwa ujumla mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya mikoa ya Dar es Salaam, Zanzibar, Tanga, Pwani (ikijumuisha na kisiwa cha Mafia) na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Morogoro.

Mikoa mingine ni Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara pamoja na maeneo ya Kaskazini ya Mkoa wa Kigoma (Wilaya za Kakonko na Kibondo).

"Pia ipo Mikoa ya Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki ambayo ni Arusha, Manyara na Kilimanjaro kunatarajiwa kuwa na mvua za chini ya wastani mpaka katika kipindi hicho cha vuli," alisema Chang'a.

Aidha, TMA kwa kushirikiana na wataalamu wa sekta husika katika mikutano mbalimbali wametoa ushauri wa athari zinazoweza kutokea kutokana na upungufu wa mvua kwa vipindi vya joto kali.

Dk. Chang'a, alisema katika kipindi cha msimu wa mvua za vuli upungufu wa unyevunyevu katika udongo unatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi yanayopata mvua hizo na kuathiri ukuaji wa mazao.

"Katika kipindi hiki wadudu na magonjwa ya mazao yanatarajiwa kuongezeka katika msimu hivyo kuathiri uzalishaji wa mazao. Vilevile, upatikanaji wa mazao ya misitu kama vile asali unatarajiwa kuathirika kutokana na uhaba wa maji na maua," alisema Dk. Chang'a.

Pia athari za ukosefu wa mvua zinatarajiwa kwenye sekta ya mifugo na uvuvi ikiwa pamoja na ukosefu wa maji na malisho na chakula kwa ajili ya samaki na kuathiri uzalishaji wa mifugo na samaki.

Aidha, katika msimu huu, magonjwa kwa mifugo yanayoenezwa na kupe pamoja na wadudu warukao yanatarajiwa kupungua.

Kukosekana kwa mvua kunaweza kusababisha upungufu wa umeme na mamlaka husika zinapaswa kuchukua hatua ya tahadhari katika kipindi hicho.

Aidha, baadhi ya magonjwa ya wanyamapori yanayotokana na upungufu wa mvua yanaweza kutokea na kusambaa kutoka kwa wanyamapori kwenda kwa binadamu, kutokana na mwingiliano.

Dk. Chang'a, alisema usafirishaji hususan wa ardhini unaweza kunufaika kutokana na vipindi vya ukavu vinavyotarajiwa.

Hata hivyo, inashauriwa kuwa kwa kipindi husika mipango ya uboreshaji wa miundombinu ya usafirishaji ifanyike kwa kuzingatia taarifa za utabiri wa hali ya hewa uliohusishwa katika eneo husika.

Pia, alisema katika sekta ya afya, hali ya upungufu wa upatikanaji wa majisafi na salama inaweza kujitokeza na kusababisha magojwa ya mlipuko katika maeneo husika kama vile vikope, magonjwa ya ngozi, kipindupindu na homa ya matumbo, changamoto za kupumua na magonjwa yanayohusiana na joto kali.

"Mamlaka husika zinashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari hasi, ikiwa ni pamoja na kuhimiza wananchi kutibu maji kabla ya kunywa, kusafisha matunda, kunywa majisafi, salama na ya kutosha ili kuepuka upungufu wa maji mwilini sambamba na kuzingatia usafi wa mwili na mazingira," alisema na kuongeza kipindi cha mvua za vuli katika maeneo mingi yaliyotajwa kinatarajiwa kumalizika wiki ya nne ya mwezi Desemba.




Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), Dk. Ladislaus Chang'a akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, kuhusu utabiri wa msimu wa mvua za vuli. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

# Bilioni 840/- kutumika ujenzi miundombinu iliyoharibiwa na El-Nino, Kimbunga Hidaya

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa ameeleza kuwa serikali tayari imeelekeza Sh. bilioni 840 (Dola za Marekani milioni 325) katika ujenzi wa miundombinu ya barabara, madaraja na makalvati yaliyoharibiwa na mvua kubwa ya El-Nino na Kimbunga Hidaya ambapo maandalizi ya utekelezaji huo yanaendelea.

Amesema kuwa kutokana na mvua ya El-Nino iliyonyesha katika kipindi cha mwezi Septemba 2023 hadi Aprili 2024 na kuathiri mawasiliano ya barabara na madaraja, serikali ilitoa Sh. bilioni 72.1 kufanya matengenezo ya dharura katika maeneo yaliyokatika mawasiliano.

Bashungwa aliyasema hayo mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu jana wakati akiwasilisha taarifa ya mkakati wa serikali kuhusu ukarabati wa miundombinu ya barabara iliyoharibiwa na mvua ya El-Nino na Kimbunga Hidaya.

"Wizara imeona umuhimu wa kuanza ujenzi wa madaraja na makalvati kwa kuwa mvua inaponyesha pindi kunapokuwa na barabara mawasiliano yanaendelea kuwepo hata kama ni kwa shida lakini daraja ama kalvati linapovunjika linasababisha mawasiliano kukosekana kabisa," alisema Bashungwa.

Waziri Bashungwa aliongeza kuwa serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ili kuhakikisha miundombinu yote iliyoathiriwa inafanyiwa matengenezo ili irudi katika hali yake ya awali ambapo tathmini ilionesha Sh. trilioni 1.07 zinahitajika kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu yote iliyoathiriwa.

Alielekeza Wakala ya Barabara (TANROADS) kuhakikisha unafanya mapitio mapya ya barabara zilizofanyiwa usanifu miaka ya nyuma ili kutekeleza ujenzi na matengenezo kulingana na uhalisia, mabadiliko ya mazingira, ongezeko la watu na ukuaji wa miji.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Selemani Kakoso, alishauri Wizara ya Ujenzi kushirikisha wabunge katika maeneo yaliyolengwa ili utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja iliyoathiriwa ufanyike kwa tija na mahitaji halisi ya maeneo husika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kurasimisha biashara kunaepusha kunyanyaswa masoko kimataifa

**MACHI** 21, 2018, nchi za Afrika zilisaini mkataba wa makubaliano ya Eneo Huru la Biashara (AfCFTA), ambalo linakadiriwa kuwa na watu zaidi ya bilioni 1.2 na pato la dola za Marekani trilioni 2.5 kwa mwaka.

Vipo vigezo ambavyo vitawawezesha wafanyabiashara wa Tanzania kulifikia soko hilo na masoko mengine ya kimataifa ambayo yanaruhusu nchi nyingine kuuza huduma na bidhaa zake nchini.

Moja ya kigezo ni kuwa na biashara iliyosajiliwa ambayo inatunza kumbukumbu zake za kifedha, mauzo, ununuzi, uzalishaji (kwa wenye viwanda), na namna wafanyabiashara wanavyozingatia ajenda ya dunia ya maendeleo endelevu kwa sekta zote.

Hapa nchini, zipo mamlaka na taasisi zinazoratibisha masuala ya biashara na kuthibitisha uhalali wake, ambazo ni muhimu wananchi wazitumie kikamilifu ili AfCFTA na masoko mengine yawanufaishe Watanzania.

Moja ya taasisi hiyo ni Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), ambayo inasajili kampuni, majina ya biashara, nembo za biashara, leseni za viwanda, miliki ubunifu na uvumbuzi (hataza).

Takwimu za BRELA zinaonyesha kwamba ni Watanzania wachache wanaomiliki biashara changa, ndogo na za kati wanaoona umuhimu wa kuzisajili. Kibaya zaidi ni kwamba ni wavumbuzi wachache zaidi, wanaojisajili kwa wakala huo.

Jambo la kusikitisha ni kwamba gharama za kujisajili zinahimilika ukilinganisha na hasara ambayo mtu anaweza kuipata kwa kutoilinda biashara yake kisheria.

Mathalani, kiwanda kidogo chenye mtaji wa chini ya Sh. milioni 10, kinachosindika unga, viungo au kinazalisha mafuta kinasajiliwa kwa Sh. 50,000 inayolipwa mara moja tu katika uhai wake wote.

Kwa wavumbuzi, ada ni Sh. 22,000 inayolipwa kwa awamu mbili na Sh. 4,000 kila mwaka baada ya kusajiliwa. Hiki ni kiasi kidogo ambacho bila shaka, Mtanzania mwenye nia ya kufanya biashara kwa uaminifu, anamudu kuilipa.

Kama tunavyofahamu, mazingira ya Afrika kwa maana ya changamoto zinazoikabili jamii zinafanana kwa kiasi kikubwa; inasikitisha kuona mtu anabuni kitu kinachoweza kutatua changamoto kwenye jamii, anakiweka mtandaoni, anakipa na jina, bila kulinda jina wala uvumbuzi wenyewe.


Hali ni hiyo hiyo wakati wa maonyesho ya biashara kama ya Kimataifa ya Sabasaba ambayo yako mbioni kuanza; unakuta mbunifu anaeleza hatua kwa hatua namna alivyofanikiwa kubuni zana fulani ya kuwasaidia wakulima au wananchi katika sekta muhimu, baada ya maonyesho hanufaiki na ubunifu wake kwa kuwa wajanja wachache wanaamua kwenda kuisajili BRELA na kuanza kuizalisha. Hii ni hasara sio kwake pekee bali kwa nchi pia.

Mpango wa serikali wa kuboresha mazingira ya biashara nchini umeweka njia rahisi za kujisajili ambayo ni kupitia mtandao (ORS), unapata huduma zote za kurasimisha biashara yako ukiwa sehemu yoyote yenye intaneti.

Tunaeleza haya ili kuukumbusha umma kwamba wajasiriamali wetu wanaweza kuzalisha bidhaa nzuri, kutoa huduma bora, tukajitangaza mtandaoni lakini mwisho wa siku, tutakuta kile tunachouza kimelindwa kisheria na mtu mwingine; ambaye atakuruhusu kuendelea kutumia nembo au jina ulilobuni, kwa kumlipa mamilioni ya fedha kwa kuwa tu ameshajisajili.

Sheria itamlinda ambaye ameitii. Hata kama utakuwa mwanzilishi wa huduma, jina, uvumbuzi au nembo, usipoisajili halafu akatokea mgeni akaisajili nchini, hutaweza kujitetea kwa sababu hutambuliki kwenye mifumo ya kisheria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Dira yetu inahitaji maoni yetu sote

Na Sabato Kasika

**DIRA** ya taifa ya maendeleo ni taswira na maono yanayohusu mustakabali unaotarajiwa wa maendeleo ya nchi kwa miaka ya mbele, kuanzia leo hadi 2050.

Dira ya 2050, inaandaliwa sasa na ndicho chungu cha kupika mipango ya maendeleo kwa miaka mingine 25 inayokuja.

Njia mojawapo ya kuchukua hatua za kuchochea maendeleo, ni kila Mtanzania kushiriki, kutoa maoni ambayo yatachangia kuifanya dira hiyo iwe shirikishi na inayohusisha kila mmoja bila kujali anaishi mjini au kijijini.

Katika kufanikisha hilo, kwa sasa wananchi wanashirikishwa kwenye makongamano, semina na warsha ambazo ni njia mojawapo za kurahisisha kukusanya maoni yao.

Kwa njia hiyo ya kukusanya maoni ya wadau, ni wazi serikali imeweka mazingira rafiki kwa makundi mbalimbli ndani ya jamii ili kuyawezesha kutoa kila wanachowaza kuwa kinahitajika kuingizwa kwenye dira ya 2050.

Hivyo, ni vyema wananchi wakatambua kuwa wako huru kutoa kutoa maoni yao na mapendekezo ya jinsi gani ambavyo wanadhani serikali inaweza kufanya ili nchi ifikie maendeleo wanayoyataka.

Maoni ya wananchi yana umuhimu kwani yataiwezesha serikali kuangalia mafanikio na mapungufu ya dira iliyopita na kuchukua hatua za kuiboresha mpya inayoandaliwa ili kusonga mbele zaidi kimaendeleo.

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inahusu maendeleo yetu, hivyo, kila Mtanzania hana budi kutambua umuhimu wake na kushiriki kutoa maoni kwa ajili ya kuiboresha dira, kwa maendeleo ya baadaye.

**Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inahusu maendeleo yetu, hivyo, kila Mtanzania hana budi kutambua umuhimu wake na kushiriki kutoa maoni kwa ajili ya kuiboresha dira, kwa maendeleo ya baadaye.**

Jambo la kuzingatia ni kwamba, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, ni taswira na maono kuhusu mustakabali unaotarajiwa wa maendeleo ya nchi siku za usoni katika kipindi kingine cha miaka 25 ijayo.

Maandalizi ya dira ni moja ya njia za kupanga maendeleo ya taifa ili liweze kustawi. Hivyo, wananchi ndio wachocheaji wa maendeleo kwa kutoa maoni ili kufikia kiwango kinachotarajiwa katika siku za usoni.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri Mkuu, Dotto Biteko, kupitia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Tanzania imepiga hatua kubwa ikiwamo kuingia kwenye orodha ya nchi ya uchumi wa kipato cha kati cha chini mwaka 2020 baada ya kufikisha wastani wa kipato cha mtu cha Dola za Kimarekani 1,080.

Hivyo, ni muhimu wananchi kuendelea kushiriki katika kutoa maoni, hasa wakati huu wa maandalizi ya dira 2050 kwa kuangalia uhalisia ili kuuliza maswali ili kujua nini kimesababisha kufikia hatua hiyo na nini kifanyike ili kupiga hatua zaidi kwenye dira hiyo mpya.

Ninaamini kuwa kwa njia hiyo, itakuwa rahisi kujikwamua ili kufikia viwango vya juu vya kipato pamoja na ustawi wa maendeleo ya kila Mtanzania na taifa kwa ujumla.

Kwa sasa vipo baadhi ya vikundi ndani ya jamii ambavyo, vimeanza kuhamasisha wananchi kutoa maoni kuhusu dira hiyo, faida za kutoa maoni ili waweze kujitokeza kwa wingi kushiriki zoezi hilo.

Miongoni mwa vikundi hivyo, ni cha Sauti ya Jamii Kipunguni Dar es Salaam, ambacho kimepanga kufikia watu 1,350 na kuwafundisha kutoa maoni, kwa njia ya simu ambayo baadaye yatachakatwa.

Watakaofikiwa na kikundi hicho, ni vyema watumie nafasi hiyo kikamilifu kutoa maoni yao ambayo huenda yakawa na mchango mkubwa, katika kuboresha dira kwa maendeleo endelevu.

## NSSF yachangamkia fursa ya elimu hifadhi ya jamii tamasha Kizimkazi

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, amesema Maonesho ya Tamasha la Kizimkazi 2024 kwa upande wa NSSF ni fursa kwa sababu ya kukutanisha watu kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Amesema Mfuko unapata fursa ya kutoa elimu ya hifadhi ya jamii kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi pamoja na kuangalia uwekezaji.

Mshomba alisema hayo Agosti 20 baada ya kufungwa kwa mafunzo ya Tamasha la Kizimkazi 2024, yaliyofanyika katika Uwanja wa Mwehe, Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja.

Aidha, Mfuko ulitoa hundi ya Sh. milioni 50 kwa ajili ya kuunga mkono shughuli za kilimo biashara.

Mshomba alisema NSSF inatumia fursa ya matamasha kama la Kizimkazi kwa sababu ina jukumu la kuifikia sekta rasmi na isiyo rasmi ambayo imebeba kundi kubwa likiwamo la wakulima, wavuvi, wafugaji na wajasiriamali wengine.

Kadhalika, amewahakikishia Watanzania kuwa, NSSF imedhamiria kuwafikia wajasiriamali wa maeneo mbalimbali nchini ili kuwapatia elimu ya hifadhi ya jamii na kujiunga na Mfuko.

"Nazidi kuwahakikishia Watanzania kuwa NSSF tuna dhamira ya dhati ya kuwafikia vijana hususani wajasiriamali nchi nzima na kuwapa elimu ya hifadhi ya jamii, kuwaandikisha ili waweze kujiwekea akiba kwa maisha yao ya sasa na ya baadaye," alisema Mshomba.

Amehakikisha kuwa NSSF itaendelea kufikisha elimu ya hifadhi ya jamii kwa makundi mbalimbali yaliyopo katika sekta binafsi na zisizo rasmi kwani hiyo ndiyo azma ya msingi ya kuandikisha Watanzania wengi ili wanufaike na sekta ya hifadhi.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa upanuzi wa Barabara ya Morogoro, eneo la Kimara Resort, Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Kanzidata ajali za barabarani, matibabu ya awali kuanzishwa

**Na Christina Mwakangale**

TANZANIA inatarajia kuwa na kanzidata za ajali za barabarani, kuboresha huduma za matibabu ya awali kwa waathirika pamoja na kuifanya elimu ya usalama barabarani shuleni kuwa tabia na mazoea kwa wanafunzi.

Hayo yalibainika jana wakati Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA) na Wizara ya Ujenzi wanatia saini kutekeleza Mradi wa Kuimarisha Usalama Barabarani utakaoanza Februari mwakani hadi Januari 2028.

Mradi huo pia unashirikisha wadau wengine kama vile Jeshi la Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani; Hospitali ya Rufani ya Mkoa Amana; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Ofisi ya Mkuu Dar es Salaam na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Wengine ni Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS); Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA).

Mradi huo unalenga kuimarisha usalama barabarani baada ya Serikali ya Tanzania kuwasilisha ombi kwa Serikali ya Japan Agosti 2023.

Mkurugenzi wa Kitengo cha Usalama na Mazingira wa Wizara ya Ujenzi, Musa Kashinde, alisema: "Tunashukuru kwa mradi wa ushirikiano wa kitaalamu kutoka JICA, na tunatarajia utaanza kwa ufanisi."

Mkurugenzi wa Timu ya Kwanza, Kikundi cha Usafirishaji cha Idara ya Usimamizi wa Miundombinu, Makao Makuu ya JICA Tokyo, Suhara Yasuhiro, alisema JICA inajitolea kufanya kazi pamoja na Serikali ya Tanzania kukabiliana na changamoto za usalama barabarani kwa manufaa ya nchi na watu wake.

Alisema mradi unalenga kuanzisha kanzidata za ajali za barabarani na kuboresha uwezo wa uchambuzi wa wadau wa usalama barabarani.

Kuboresha huduma za matibabu ya awali kwa waathirika wa ajali za barabarani na kuongeza uwezo wa utekelezaji hatua za kina zinazolenga elimu ya usalama barabarani shuleni.

Mradi huo unatarajiwa kupunguza ajali kwa kuendesha programu za kutoa elimu kwa umma, hasa kwa madereva vijana kuhusu usalama barabarani.

Pia, madereva na watembea kwa miguu ambao wana uelewa kuhusu usalama barabarani, wawajibike kwa kufunga mikanda ya usalama safarini na kufuata viwango vya kasi na kuepuka vitu vinavyovuruga umakini.


Jamii itahusishwa katika elimu ya usalama barabarani na changamoto zake kushughulikiwa, hivyo kuwa na programu za usalama zilizoboreshwa na zenye ufanisi zaidi.

Mradi huo unasisitiza kuwapo mfumo wa dharura, ulio na uratibu mzuri ambao utapunguza kwa kiasi kikubwa uzito wa majeraha na vifo katika tukio la ajali barabarani na kuhakikisha matumizi bora ya dharura kama vile magari ya wagonjwa na watoa huduma ya kwanza.

JICA imekuwa inaunga mkono sekta ya usafirishaji nchini kwa zaidi ya miaka 40 na mradi wa kwanza wa miundombinu ulikuwa ni ujenzi wa Daraja la Selander kutoka mwaka 1980 hadi 1982.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Vijana wahamasika kujiandikisha Daftari la kudumu la wapigakura

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

WAKAZI wa mikoa ya Mwanza na Shinyanga wamejitokeza kwa wingi katika siku ya kwanza ya Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ulioanza juzi na hadi Agosti 27.

Mwandishi wa habari hii, ameshuhudia wananchi wengi vituoni hasa vijana na wanawake waliojitokeza kujiandikisha na kuboresha taarifa zao katika daftari hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati akitoa tathmini ya mwenendo wa daftari hilo kwa siku ya kwanza Mkoa wa Mwanza, Mjumbe wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, ambaye pia ni Jaji wa Mahakama Kuu, Asina Omari, amesema uboreshaji umeanza vizuri na mwitikio wa wananchi ni mkubwa.

"Leo (juzi) siku ya kwanza zoezi limeanza vizuri ambapo wananchi wamejitokeza, mawakala wapo vituoni na nimebahatika kuzungumza na mawakala, watendaji vituoni na wananchi kwa ujumla zoezi linakwenda vizuri," alisema Jaji Asina.

Aidha, Jaji Asina alisema changamoto zilizojitokeza ni za kawaida na zinatatulika, lakini kubwa ni wananchi wanaofika kuboresha taarifa zao kusahau majina waliyoyatumia awali kujiandikishia namna ya wanavyoandikwa kwa usahihi na kusababisha uchelewaji vituoni.

Alisema makundi maalum ya wajawazito, wanaonyonyesha na kufika na watoto wao vituoni, wazee, wagonjwa na wenye ulemavu wameendelea kupewa kipaumbele kama Tume inavyosisitiza.

Jaji Asina alitembelea baadhi ya vituo katika majimbo ya Magu, Nyamagana na Ilemela na kuwasihi wananchi kuendelea kujitokeza kwa wingi kwa siku sita zilizobaki.

"Niwasihi wananchi wajitokeze katika vituo ili waweze kujiandikisha na kuboresha taarifa zao ambapo katika vituo tumeona vijana wengi, hivyo watumie siku hizi zilizobaki kuboresha taarifa zao na kujindikisha," alisema Jaji Asina.

Mjumbe wa Tume, Balozi Omar Ramadhan Mapuri, ambaye yupo mkoani Shinyanga, alisema uboreshaji umeanza vizuri na wananchi wengi wamejitokeza kujiandikisha kwa wingi.

Mawakala wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Paul Msafiri na Wakala wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Lydya Martin waliopo kituo cha Bulola Mlimani kilichopo eneo la Zahanati ya Nyerere Halmashauri ya Ilemela, wamesema kazi inakwenda vizuri na hakuna changamoto iliyojitokeza.

Aidha, wakala Fatuma Athumani wa Chadema aliyepo kituo cha Miembeni A kilichopo eneo la wazi Nyakabungo A katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza aliwahimiza wananchi kujitokeza kwa wingi kupata haki yao kupewa kadi ya mpigakura.

Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa mikoa ya Mwanza na Shinyanga umeanza Agosti 21 hadi Agosti 27, 2024 na Tume inatarajia kuandikisha wapiga kura wapya 400,082 kwenye mikoa hiyo.

Mkoani Mwanza wapiga kura wapya 190,131 wataandikishwa huku Shinyanga wapiga kura wapya wanaotarajiwa kuandikishwa ni 209,951.



Baadhi ya wakazi wa Jiji la Mwanza, wakiwa wamepanga foleni kwa ajili ya kujiandikisha na kuboresha taarifa zao katika Kituo cha Kuboreshea Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, jijini humo juzi. **PICHA: INEC**

# Madaktari Congo DRC waja kujifunza JKCI

**Na Joseph Mwendapole**

MADAKTARI wanane kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), wanatarajiwa kutembelea Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), kwa ajili ya kujifunza ilivyopiga hatua katika tiba ya moyo na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali kwenye vifaa tiba na wataalamu bobezi.

Mkurugenzi wa Global Medicare iliyoratibu ziara hiyo kwa kushirikiana na JKCI, Abdulmalik Mollel, alisema jana kuwa madaktari hao wanatoka katika hospitali kubwa ya rufani ya Ngaliema mji wa Kinshasa.

Alisema ujumbe huo utaongozwa na Dk. Kongo Minga, ambaye ni Mkurugenzi wa Hospitali ya Ngaliema na kwamba ziara hiyo inatarajiwa kufanyika JKCI kuanzia Agosti 26 hadi 31.

"Hii ikiwa ni mara ya kwanza kwa madaktari hawa kutoka Congo DRC kufika Tanzania kufanya ziara hii yenye dhamira ya kuzuru katika hospitali zetu kuona uwekezaji wa sekta ya afya hasa ya matibabu ya moyo uliofanyika na Serikali ya Tanzania watakuja kuona namna serikali yetu ilivyofanya mambo makubwa kwenye sekta ya afya husussan tiba ya moyo kwa kuweka mitambo ya kisasa ya tiba ya moyo," alisema.

Alisema ziara ya madaktari hao inatokana na uwekezaji mkubwa wa serikali kwa taasisi ya JKCI ambayo ina madaktari bingwa wa kutosha wa moyo kwa watoto na watu wazima na mitambo mbalimbali ya kisasa ambayo ni sawa na iliyoko kwenye hospitali za nchi zilizoendelea ikiwamo mitambo miwili ya Cathlab.

Alisema ziara hiyo itasaidia kuendeleza uhusiano mwema kati ya Tanzania na Congo DRC katika kuboresha matibabu ya moyo ikiwa na dhamira ya kujengeana uwezo wa kimatibabu hasa ya moyo.

Aidha, alisema ziara hiyo inakuja baada ya timu ya madaktari na wawakilishi kutoka JKCI na Muhimbili kwenda nchini Congo katika ziara ya kitabibu Ngaliema, Kinshasa mwezi Mei, mwaka huu.

"Madaktari wa JKCI na Muhimbili walitembelea hospitali za Congo DRC na walijenga uhusiano mzuri kama taasisi za kitabibu hivyo ziara hii inayotarajiwa kuanza Jumatatu ni chachu kwa sekta yetu ya afya ikiwa Tanzania inajikita kuwa kitovu cha tiba utalii kati ya nchi za kusini mwa Sahara," alisema.

"Tunajivunia uwekezaji mkubwa wa serikali yetu katika vifaa tiba na rasilimali watu kuboresha huduma za afya hivyo ujio wa madaktari hawa ni sehemu ya kutengeneza uhusiano mzuri na nchi jirani, lakini pia kutangaza matibabu bora yanayopatikana Tanzania," alisema Mollel ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Tiba Utalii Taifa.

## Kamati ya bajeti Z'bar yaridhishwa utendaji TCRA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imeeleza kuridhishwa na kazi inayofanywa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuimarisha mawasiliano na kusambaza teknolojia ya 5G.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mwanaasha Khamis Juma, aliyasema hayo wakati wa ziara ya siku moja kufahamu kazi na usimamizi sekta ya mawasiliano zinazofanywa na mamlaka hiyo katika ofisi zake za Dar es Salaam.

Alishukuru TCRA kwa kuendelea na jitihada zake za kuhakikisha kuwa miundombinu ya 5G inasambazwa kwa kasi na ufanisi zaidi.

"Teknolojia hii ya kisasa ina uwezo wa kuboresha mawasiliano ya intaneti kwa kasi zaidi, hivyo kufungua fursa nyingi za kibiashara, huduma za afya, na elimu kwa njia ya mtandao," alisema.

Mwanaasha alisema 5G itasaidia kuimarisha ukuaji wa sekta mbalimbali kama vile kilimo, viwanda, na uchukuzi.

Aidha, kamati hiyo iliitaka TCRA kuendelea kuhamasisha matumizi ya namba hiyo ili kuhakikisha kuwa uhalifu mtandaoni unadhibitiwa kwa ufanisi zaidi, huku wakipongea uamuzi wa kuwa namba maalum ya kuripoti utapeli ya 15040.

Akiwakaribisha wanakamati hao, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Philip Filikunjombe alisema usambaaji wa teknolojia ya 5G unazidi kuenea nchini

"Kwasasa tuna minara 638 ya 5G ambayo ni sawa na asilimia 15 ikiwa ni ongezeko la asilimia mbili toka robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2023/24," alisema.

Kuhusu hali ya usalama na udhibiti wa matukio ya utapeli, Dk. Filikunjombe alisema ripoti ya TCRA ya robo mwaka ya mwisho ya mwaka wa fedha 2023/24, inaonesha kuwa mifumo ya udhibiti imebaini majaribio ya uhalifu mtandaoni 22,257.

"Hii inaonesha ubora wa mifumo hiyo katika kubaini na kudhibiti jumbe za kilaghai zilizotumwa na matapeli," alisema.

Kuhusu ujenzi wa jengo jipya la TCRA Zanzibar, alisema litakuwa ni kitovu cha shughuli zote za udhibiti wa mawasiliano visiwani hapo na litasaidia kuimarisha ufanisi wa mamlaka hiyo katika kutoa huduma zake kwa wananchi.

"Ujenzi huu pia unalenga kuleta urahisi katika usimamizi wa masuala ya mawasiliano na kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma bora zaidi. Kamati hii inaahidi kutembelea eneo la mradi ili kujionea maendeleo ya ujenzi, pia tutashauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), kusaidia katika ujenzi huu pale itakapobidi," alisema Mwenyekiti wa kamati.

Mjumbe wa kamati, Prof. Omari Fakhi Hamadi, alisema ni muhimu TCRA ikaimarisha elimu ya matumizi bora ya mitandao kutokana na ukuaji wa teknolojia ili wananchi watumie mitandao kwa usalama na manufaa.

"Elimu hii itasaidia kupunguza hatari za uhalifu mtandaoni na kuimarisha usalama wa watumiaji wa mitandao," alisema.



## Mgambo kusaka wafugaji kwa kukaidi kulima choroko

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI ya Wilaya Monduli mkoani hapa imewaagiza wanaume wa jamii ya wafugaji kufanya maandalizi ya kilimo cha choroko na mbaazi katika msimu ujao ili kuinua uchumi wao.

Agizo hilo lilitolewa jana na Mkuu wa Wilaya hiyo, Festo Kiswaga wakati akizungumza na wananchi katika Kijiji cha Mswakinikuhusiana na umuhimu wa kujikita katika kilimo hicho badala ya kutegemea mifugo kuendesha maisha yao.

" Wenzenu hapo Babati mkoani Manyara, wananufaika na mazao ikiwamo mbaazi kwa kuwa kilogramu moja inauzwa Sh. 3,500 na ardhi yenu ni sawa na ya Babati inakubali mazao haya, hivyo nawaagiza wanaume na vijana msimu wa kilimo ukianza sitaki kukuta mtu nyumbani ni shambani na mpende msipende," alisema.

Alisema ameandaa kikao cha viongozi wa vijiji ili kuhakikisha agizo hilo linatekelezwa katika maeneo yao.

" Hapa sitanii naandaa askari mgambo ambao watapita kukagua nyumba kwa nyumba, kuhakikisha hakuna mwanaume na kijana anakaa nyumbani wakati wa kilimo ni lazima tukubali kubadilika," alisema Kiswaga.

Alisema wafugaji wa jamii hiyo wamezoea wanapopata tatizo katika familia zao hata kama chumvi imeisha kutatua mpaka wakamate mfugo wauze, kisha wakanunue .

Kiswaga alisisitiza kuwa, atahakikisha elimu hiyo inapelekwa katika vijiji vyote 62 ili utekelezaji wake uwe rahisi

"Kila mtu ahakikishe analima zao la mbaazi ekari mbili na choroko ekari mbili na mtanikumbuka, nawalazimisha kulima lakini mkivuna siwaingilii kila mtu anatumia atakavyo fedha zake," alisema.

## Meru watekeleza miradi ya maendeleo

**Na Allan Isack,** ARUMERU

HALMASHAURI ya Meru wilayani hapa Mkoa wa Arusha imetekeleza miradi ya maendeleo yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 1,8 kwa kipindi cha miaka mitatu kwa fedha za mapato ya ndani.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Zainabu Makwinya wakati akizungumza na watendaji wa vijiji na kata kuhusu mrejesho wa kazi zilizofanywa na halmashauri kwa kipindi hicho.

Makwinya, alisema fedha hizo zimefanikisha utekelezaji wa miradi hiyo ikiwamo elimu ya: sekondari, msingi na sekta ya afya.

Alisema lengo la kutoa tathmini hiyo ni kuonesha namna serikali ilivyoisadia Meru kuongeza ufanisi wa kuwahudumia wananchi wake.

Akizungumzia kuhusu ukusanyaji wa mapato, alisema yameongezeka hadi kufikia Sh. bilioni 10 kutoka Sh. bilioni 6.1.

Aidha, Makwinya aliwataka watendaji wa kata na vijiji kusimamia ukusanyaji wa mapato katika maeneo yao kwa ajili ya kuwaletea wananchi maendeleo.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Emmanuela Kaganda, alimpongeza mkurugenzi huyo kwa usimamizi mzuri wa miradi ya maendeleo ya halmashauri hiyo

# Samia atoa motisha kwa wanaohama Ngorongoro

**Na Mwandishi Wetu,** NGORONGORO

RAIS Samia Suluhu Hassan, ametoa fedha ya fidia na motisha ya maendelezo yake kwa kila kaya iliyokubali kuhama kwa hiari ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Sh. milioni 10 ili kupisha shughuli za uhifadhi.

Uamuzi huo wa Rais Samia, unalenga kuwapa hamasa wananchi hao kujenga nyumba nyingine mbadala tofauti na zile za vyumba vitatu wanazopewa na serikali.

Ofisa Uhifadhi Mkuu na Meneja Mradi wa kuhamisha wananchi kwa hiari, Flora Assey, aliyasema hayo jana katika Wilaya ya Ngorongoro, mkoani Arusha, wakati Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Benedict Wakulyamba akiongoza zoezi la kuwaaga wananchi wengine 367 waliokubali kuhama makazi yao kwa hiari kupisha hifadhi hiyo.

"Mwitikio wa wananchi wanaoishi ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kuendelea kuhama kwa hiari unaendelea kwa kasi.

Hadi kufikia leo (jana), kaya 79 zenye watu 367 na mifugo 995 zimehama kutoka Ngorongoro kwenda Kijiji cha Msomera, Kata ya Misima, Wilaya ya Handeni na maeneo mengine waliyochagua wenyewe," alisema.

Awali, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi, Daniel Chegere, alisema NCAA inaendelea kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kuhama kwa hiari kwenda maeneo yaliyotengwa na serikali baada ya kujengewa miundombinu ya kisasa yenye huduma muhimu za jamii na usalama zaidi tofauti na ilivyo ndani ya hifadhi hiyo.

Chegere, alisema hali ya usalama katika hifadhi hiyo inaendelea vizuri, ulinzi umeimarishwa na wageni wanaotembelea vivutio wanaendelea na shughuli za utalii bila changamoto.

Kwa upande wake Wakulyamba, alisema kuondoka kwa kundi hilo ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa kulinusuru eneo la hifadhi hiyo.

Alisema wananchi wameendelea kuelimishwa na kuhama kwa hiari kwa ajili ya kuboresha maisha yao na kunufaika na fursa za kiuchumi zilizoko nje ya hifadhi.

Kuanzia Juni mwaka 2022 hadi kufikia mwezi huu, takriban kaya 1,598 zenye watu 9,618 na mifugo 39,779 zimehama ndani ya hifadhi hiyo kwenda Msomera mkoani Tanga na maeneo mengine.



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Lushoto, Japhari Kubecha (kulia), akikabidhi rasmi ofisi kwa Mkuu mpya wa Wilaya hiyo, Zephania Sumaye, katika Halmashauri ya Lushoto, mkoani Tanga mapema wiki hii. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# Kaya maskini 59,904 zapewa bilioni 2.5/-

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 2.5 kwa kaya 59,904 mkoani hapa kupitia mpango wa kunusuru kaya masikini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) nchini.

Kwa mujibu wa Mratibu wa TASAF Mkoa wa Arusha, Richard Nkini, mgawo huo wa fedha umezingatia kaya zilizoko kwenye mpango kwa kila halmashauri mkoani hapa.

Nkini alitaja kiasi cha fedha na halmashauri kwenye mabano kuwa Shilingi milioni 551.6 zimegawiwa kwa kaya 13,795 (Arusha), Shilingi milioni 174.6 kaya 4,385 ( Jiji la Arusha) na shilingi milioni 328.9 kaya 7,761 (Karatu).

Alisema Shilingi milioni 318 kaya 7,177 (Monduli), Shilingi milioni 447.1 kaya 10,111 (Ngorongoro), Shilingi milioni 301.6 kaya 7,769 (Meru) na Shilingi milioni 388.9 kaya 8,905 (Longido).

Nkini alisema lengo la serikali kugawa fedha hizo ni kuziwezesha kaya hizo kujiinua kiuchumi na kijamii kupitia miradi inayotekelezwa na TASAF, ikiwa ni pamoja na ya vikundi vya kuweka, kuwekeza na kukopa.

TASAF ni mpango wa serikali unaolenga kusaidia kaya masikini nchini kupitia uwasilishaji fedha moja kwa moja kwa walengwa.

"Mpango wa TASAF ni jitihada za serikali za kupunguza umaskini na kukuza maendeleo ya jamii na kupitia programu ya kutoa fedha moja kwa moja kwa walengwa ili kuongeza upatikanaji wa huduma za msingi kama elimu na afya na kuboresha uwezo wa kaya hizo kujikimu kiuchumi," alisema.





# Wananchi waomba kushirikiana Polisi kudhibiti uhalifu Mwanza

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAKAZI wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, wameombwa kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi ili kudhibiti vitendo vya uhalifu.

Ombi hilo lilitolewa juzi na Naibu Meya wa Jiji hilo, Biko Kotecha wakati akizungumza na wafanyabiashara na abiria kivuko cha Kamanga wakati wa mkutano wa hadhara ulioitishwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilbrod Mutafungwa.

"Jukumu la ulinzi ni letu sisi sote si Jeshi la Polisi pekee, ukichukua wananchi wote wa Jiji la Mwanza kila askari awe na mtu mmoja haitawezekana lazima sisi tuwasaidie tuwe nao pamoja," aliseme Kotecha ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Nyamagana.

Dominic Domisian, dereva bodaboda wa Kituo cha Kamanga Feri, licha ya kuahidi ushirikiano na jeshi hilo, alisema operesheni ya kuzuia uhalifu hususani makosa ya usalama barabarani imekuwa msaada wa kuleta utulivu jijini Mwanza.

Kamanda Mutafungwa, alisema mkutano huo ni mkakati wa jeshi hilo kuanza kusikiliza na kutatua kero kwa wananchi waishio maeneo ya kando ya Ziwa Victoria ili kuhakikisha wanafanya shughuli zao katika hali ya usalama.

Alisema amefurahi kuona imani kubwa ya wananchi kwa jeshi hilo kwa kujitokeza kwa wingi katika mkutano huo ulioambatana na utoaji wa elimu ya mpiga kura.

"Ni imani kubwa ambayo mnayo kwa Jeshi lenu la Polisi, tunawapongeza sana muendelee kuwa na imani hiyo kwani ni la kwenu ambalo kazi yake ni kulinda usalama wa watu na mali zao," alisema Mutafungwa.



Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mwanza, Martin Nkwabi (kulia), akizungumza na walimu na maofisa wa elimu kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa, jijini Mwanza juzi, wakati wa kutangazwa kwa matokeo ya utimilifu kidato cha nne kwa mikoa hiyo. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Halmashauri yaagizwa kusambaza mbolea kila kata

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

HALMASHAURI ya Buchosa wilayani Sengerema Mkoa wa Mwanza, imeagizwa kupeleka mbolea ya ruzuku kila kata ili kuwaondolea wakulima adha ya kutembea umbali mrefu kufuata makao makuu.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Idama Kibanzi katika kikao cha robo ya nne kufuatia hoja iliyoibuliwa na Diwani wa Kata ya Nyakalilo, Christopher Kabugwe kuhusu mbolea hiyo kuchelewa kuwafikia wakulima.

Kibanzi, alisema msimu wa kilimo umeanza, wakulima wanahitaji mbolea ya ruzuku kwa wakati katika maeneo yao tofauti na miaka ya nyuma.

Alisema ofisa kilimo anatakiwa kuhakikisha mbolea hiyo inapelekwa ngazi ya kata ili iwafikie wakulima kwa wakati.

Awali Diwani wa Kata ya Nyakarilo, Christopher Kabugwe, alisema katika halmashauri hiyo, wakulima wanaanza kilimo mapema, hivyo mbolea hiyo inatakiwa iwe imewafikIa kwenye kata zao na si wao kufuata kwenye makao makuu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Benson Mihayo aliahidi kuhakikisha mbolea hiyo inawafikia wakula ngazi ya kata na kwa wakati ili wasichelewe kuanza kilimo.

Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga aliwataka madiwani kuhakikisha wanahamasisha wananchi kujitokeza kujiandikisha katika daftari la kudumu la mpiga kura.

# Waandishi watakiwa kuelimisha jamii

**Na Samson Chacha,** TARIME

WAANDISHI wa habari mkoani Mara wametakiwa kushiriki kikamilifu kutoa elimu ili kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya na maambukizi ya virusi vya Ukimwi katika jamii.

Wito huo ulitolewa juzi na wataalamu kutoka Shirika la CDF linalotoa huduma na elimu kwa vijana kujikinga na matumizi ya dawa hizo, maambukizi ya Ukimwi, mimba na ndoa za utotoni.

Mkufunzi wa mafunzo hayo, Anol Masawe, alisema kuwa mpango unaendeshwa na CDF kwa ushirikiana na Wizara ya Afya na nchi za Zambia, Namibia na Kenya.

Maswe, alisema kupitia vyombo vya habari wananchi wanatakiwa kufikiwa na elimu kwa wakati ili kujiepusha na matumizi ya bangi, pombe na dawa za kuzuia mimba kwa wasichana.

Ofisa Habari wa Mkoa wa Mara, Rinfrida Ngatunga, alisema jukumu la waandishi ni pamoja na

kwenda vijijini na kuwafikia walengwa wengi zaidi.

Mhudumu wa Afya kutoka Wizara ya Afya, Leah Daniel, elimu hiyo imekuwa ikitolewa kwa vikundi vya vijana katika vituo vya afya 10 wilayani Tarime.

# DAS Shy awabana madiwani, watendaji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KATIBU Tawala wa Wilaya (DAS) ya Shinyanga mkoani hapa, Said Kitinga amewataka madiwani wa halmashauri ya wilaya hiyo kushirikiana na watendaji ili kufikia malengo ya ukusanyaji mapato.

Kitinga alitoa rai hiyo katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo kilichofanyika mwanzoni mwa wiki hii.

Alisisitiza kuwa kufanya kazi kama timu ya pamoja katika suala la ukusanyaji wa mapato, kutasaidia kufikia malengo na kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao.

Akifunga kikao hicho, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ngassa Mboje alimtaka Mkurugenzi Mtendaji, Dk. Kalekwa Kasanga kuendelea kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato ya halmashauri yao.

"Mwaka wa fedha uliopita 2023/24 unaioshia Juni 30, mmevuka lengo la ukusanyaji mapato kwa asilimia 101 nawapongeza kwa hilo, ombi langu sasa kwako mkurugenzi endeleeni kudhibiti mianya yote ya upotevu wa mapato," alisema Mboje.

Akizungumza katika kikao hicho, Dk. Kasanga, alisema wataendelea na kasi hiyo ya ukusanyaji mapato ya halmashauri hiyo na kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha.

Halmashuri hiyo katika mwaka wa fedha 2023/24 imevuka lengo la kukusanya mapato Sh. bilioni 3.288 sawa na asilimia 101 hadi kufikia Juni 30, mwaka huu badala ya Sh.bilioni 3.255.

**Akifunga kikao hicho, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ngassa Mboje alimtaka Mkurugenzi Mtendaji, Dk. Kalekwa Kasanga kuendelea kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato ya halmashauri yao.**



Ukurasa 12

TENA KINA KABUDI, LUKUVI...
Kutoka turufu yake Rais kisiasa, hadi uchumi rasilimaliwatu kazini

# BUFE

IJUMAA AGOSTI 23, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ndivyo kutokurasimisha biashara zao kunavyowaweka kando kimafanikio

Ukurasa 14

# Dodoma kuwa shule ya kilimo, darasa likielimisha wakati wote

**Na Augusta Njoji, DODOMA**



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Rosemary Senyamule. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

WAKULIMA, wafugaji na wavuvi popote walipo wataanza kunufaika na mafunzo, teknolojia za kidijitali na taarifa mbalimbali watakazozichota kutoka kijiji cha kilimo jijini Dodoma.

Kijiji cha kilimo kitakachowahudumia wakulima muda wote, mwanzo hadi mwisho wa mwaka, kitajengwa wakati wowote kuanzia sasa, anasema Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Rosemary Senyamule.

Anafafanua kuwa, wakulima muda wote wanahitaji elimu ya kilimo, ufugaji na uvuvi pamoja na pembejeo ndiyo sababu ya kuanzishwa huduma kijiji hicho.

"Maonesho ya mwaka huu si kama yalivyokuwa yakifanyika miaka ya nyuma ambayo yalikuwa ni ya mazoea ya kukutana Agosti mosi hadi 8 kila mwaka. Siku zikiisha tunafungasha na kuondoka na kungoja mwaka unaofuata.

"Sasa tunakuja na kijiji cha kilimo ili elimu itolewe kuanzia Januari hadi Desemba kila mwaka, siyo kusubiria Nanenane " anasema Mkuu wa Mkoa.

Anaeleza kuwa, viwanja vya Nanenane mkoa huo utautumia kwa ajili ya utalii wa kilimo kwa kutoa fursa ya wakulima na wafugaji kujifunza mbinu za kisasa ili kuendesha shughuli zao kibiashara.

Wakati kijiji cha kilimo kitawakaribisha siku zote za mwaka na kwamba ni darasa la kujifunza mambo mapya ikiwamo teknolojia ya kisasa.

"Asilimia 72 ya wakazi wa Dodoma ni wakulima hivyo mabadiliko ya kiuchumi katika sekta ya kilimo hii yataongeza pato la mtu mmoja mmoja na mkoa tuna hamu ya kuchangia pato la taifa,"anasema.

Anaeleza kuwa, viwanja hivyo vitakuwa na kumbi za mikutano na nyumba za wageni ambazo watazitumia wakati wa kupata mafunzo.

"Viwanja vinatumika mwaka mzima vinahudumia wakulima ambao watapata mafunzo kupitia mashamba darasa sambamba na kuwapo na viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi, eneo la viwanda kuendelea kukuza mji wetu na biashara ,"anasema.

Kutajengwa kituo cha umahiri cha zana za kisasa za kilimo na wakulima watakodisha kwa mikataba.

Rosemary anabainisha kuwa, mkoa huo una ardhi yenye rutuba inayofaa kwa kilimo cha mazao mbalimbali na ni fursa muhimu kwa wakulima wa ndani na wa nje kuwekeza.

Anawaambia wenye nia katika sekta za kilimo, mifugo, na uvuvi zina mchango mkubwa katika maendeleo ya mkoa akitoa wito kwa wana Dodoma kujifunza na kubadilishana uzoefu na wataalamu mbalimbali wa sekta hizo.

Akizungumzia maonesho ya Nanenane mwaka huu Roemary anasema yamekuwa ya kipekee na yametoa matokeo chanya akimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia kufanyika kanda ya kati ambayo ni Dodoma na Singida.

"Katika maonesho hayo hakuna mdau aliyekosekana kwenye mnyororo wa thamani kuanzia kulima, kupima udogo, kupanda, kuvuna, kuchakata na kuuza sokoni,"anasema Mkuu wa Mkoa.

Yameonesha kuwa na hadhi hadi kufikia ngazi ya kimataifa kwa kuwa kulikuwa na wadau zaidi ya 50 kutoka nchi mbalimbali duniani, anasema.

"Hawa wadau wameshirikiana na wizara, mikoa na taasisi zengine kufanikisha utoaji wa elimu za sekta za kilimo, mifugo na uvuvi na kuonesha bidhaa mbalimbali za sekta hizi ambazo ni nguzo ya uchumi wetu,"anasema Mkuu wa Mkoa.

Pia, anaangazia sura ya uwanja wa maonesho akisema umefanyiwa mabadiliko makubwa kwa kujengwa na kuendelea na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya maonesho hayo.

Anasema Nanenane imechangia kubadilisha kilimo cha kujikimu na kuwa cha kibiashara kwa wana Dodoma wengi na Watanzania wa mikoa mingi.

Kuhusu miradi ya kilimo na ufugaji, Rosemary anasema ndani ya mkoa wa Dodoma kuna uwekezaji wa mradi wa kudhibiti sumukuvu unaogharimu zaidi ya Sh. bilioni 18 ambao utaifanya mkoa kuwa na soko la uhakika la mazao yenye ubora yanayokubalika kimataifa.

"Tunashuhudia mapinduzi kwenye sekta ya kilimo. Aidha, Dodoma ilikuwa inatambulika kuwa ni mkoa wenye ukame lakini kwa uwekezaji unaofanywa na serikali sasa eneo ambalo lilikuwa likipata chakula cha msaada au cha bei nafuu linakwenda kuwa mshiriki wa kufikia lengo la kuwa na usalama wa chakula wa taifa,"anaeleza Mkuu wa Mkoa.

Anaitaja miradi mikubwa ambayo serikali inatekeleza ya ujenzi wa mabwawa yatakayotumika kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwamo kilimo cha umwagiliaji kuwa ni :

Msagali utakaomwagilia ekari 20,000, Ndogoe ambao ni wa vijana wa jenga kesho iliyo bora (BBT) utakaomwagilia ekari 110,000.

Anasema upo mwingine kata ya Membe wilayani Chamwino utakaohudumia ekari 8,000 na ule wa Chinangali utakaotumiwa kumwagilia ekari 1,700..

Anauzungumzia mradi wa Bahi utakaomwagilia ekari 600 za mazao mbalimbali.

"Tunasema kilimo ni utalii, utalii wa kilimo tumeupa uzito wa kipekee tunazo Zabibu ambazo tunazitumia kuhamasisha utalii,"anasema Mkuu wa Mkoa.

Dodoma ina mengi ya kujivunia ukiwamo mradi wa kufuga mbuzi unaogharimu zaidi ya Sh. bilioni 18 na zaidi ya mbuzi 15,000 wanaouzwa kila baada ya miezi mitatu hivyo mkoa utakuwa sehemu ya wanaouza nyama katika masoko ya kimataifa.

Baadhi ya wananchi, wanaozungumzia Nanenane mwaka huu wanaungana na Mkuu wa Mkoa kuwa imekuwa ni 'darasa' lililoshe-

Inaendelea Uk 14

## UCHUMI

TENA KINA KABUDI, LUKUVI...

# Kutoka turufu yake Rais kisiasa, hadi uchumi rasilimaliwatu kazini

**Na Mwandishi Wetu**

HADI sasa taifa linaingia ndani ya mageuzi. Iko wazi, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kama ilivyokuwa katika hotuba yake fupi kwenye tukio mojawapo la kuapisha viongozi aliowateua, akawasisitizia warejee tamathali "nafasi hizo ni kama nguo za kuazima, kuachiwa kutumia, kunategemea ufanisi wao unaojumuishwa pia na nidhamu..."

Kuna wakati Rais akaanika dira ya safu yake, kwamba anawahitaji umri wenye damu ya ujana zaidi na ikashuhudiwa akiwapumzisha wazee kama kina William Lukuvi na Prof. Palamagamba Kabudi, akiahidi kuwatumia katika nafasi nyingine kwa maana ya 'utu uzima dawa.'

Kama ilivyo kawaida ya siasa, ikasikika minog'ono ya chini na kupaza sauti, vilevile kitaaluma, pia kisiasa ndio ilikuwa mingi. Ndivyo ilivyo alipofanya uteuzi uliowarejesha sebuleni siku chache zilizopita, mwanasheria Prof. Kabudi, akitumikia taaluma yake.

Mara zote ndio uhalisia wa siasa unakosimama kama wataaluma' Harold Laswel, anayeibebesha tafsiri aipendayo na kushabikiwa sana "ni nani anapata nini, lini na kwa namna gani" huku profesa mwenziwe, Mwingereza David Easton, katika ripoti ya utafiti wake ukiishia tafsiri "Siasa ni sanaa ya kuliwezesha (jambo) liwezekane..."

Hivyo ndani ya reli ya wasomi hao, unapomchimba Rais Dk. Samia, dira yake tangu akabidhiwe mamlaka ya kuiongoza nchi, mtihani wake ni 'kikokotoo' cha kumfikisha malengo ya kimaendeleo na kiuchumi aliyo nayo, ambayo nyuma ya pazia yana shinikizo la aina nne.

Inaanzia, nadhira yake binafasi juu Watanzania na maisha yao ya wanayopaswa kuwa; vilevile ana kofia ya pili ya ahadi za Chama Cha Mapinduzi (CCM), iliyoyanadi kwa umma, sasa ana wajibu wa kuyatekeleza na hivi karibuni tu wataanza kumdadisi mavuno.

Deni la tatu ambalo anaweza kulitafsiri ni la asili, kwamba wajibu wa kitaaluma wa chama chohote ni kupigania kushika madaraka ya kuongoza nchi, jambo ambalo wenzake watano walilifanikisha, awamu iliyopita akiwa sehemu yake, sasa anaiendeleza, sambamba na yaliyowekezwa kihistoria tangu uhuru wa nchi.


Sura ya nne , mbali na nafasi yake kisiasa na kiutawala, kitaaluma katika matumizi rasilimaliwatu ni eneo ambako ana stadi nazo za darasani kutoka iliyokuwa Taasisi ya Uongozi wa Maendeleo Mzumbe (IDM) miongo mitatu iliyopita (sasa chuo kikuu),yeye yuko katika katika zama za kutumikia taaluma, tena katika mawanda hayo mapana. Asipofanikisha hilo, ni kikohozi kinachomtesa nje ya siasa, ila binfasi na kwa 'ma-class mate' wake wa Advanced Diploma in Public Administration.



Rais Samia Suluhu Hassan



William Lukuvi



Palamagamba Kabudi

**MAANA YA UTEUZI**

Na katika uwekezaji wa mifumo ya utendaji katika maeneo ya mijumuiko ambako kunatakiwa rasilimali zaidi, kumegawanyika katika sura kuu mbili; mmoja ni penye huduma na kama hospitali, elimu, vyombo vya habari, ulinzi na majukumu ya serikali kwa jumla, huhitaji zaidi nguvu kazi. Ufanisi au kulegea nafasi yake kwanza huanza na rasilimaliwatu.

Upande wa pili, hasa katikia uzalisahi wa kisasa, ndio huhitaji vifaa zaidi kuliko raslimaliwatu maarufu 'capital intensive'

Pia, katika tafasiri ya jumla ya uchumi maendeleo, ambako Dk. Samia akiwa mtaalamu, madarasa mawili aliyoyapata ughaibuni na hapa nyumbani, inafafanua katika mahitaji makuu ya uchumi kama vile ardhi, mtaji, rasilimaliwatu ina nafasi kubwa, kwani mbali na kutumika, inasimamia mingine ,pia ikifanya ubunifu, ikijiendesha.

Hiyo ndio siri hata Shirika la Fedha Duniani (IMF) kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB), kuanzia katikakati ya miaka ya 1980, lilisimamia mabadiliko hayo na ndio ikawa siri ya duniani kuaza kushuhudia mabadiliko kutoka msamiati 'nguvu kazi' (personnel) hadi 'rasilimaliwatu ((human resource), na mitaala ya taaluma husika ikaanza kubadilika kimataifa kwa kasi, nchini ikishuhudiwa zaidi kasi kuanzia katikati ya miaka 1990.

Ndani ya ujumbe huo wa kitaaluma, ndio umebeba nafasi ya Rais Dk. Samia kulikoni anaonekana kuwa mkali na makini na utendaji wa umma, kukiendana na mabadiliko ndani ya mfumo wa utumishi serikalini, hadi kwenye chama. Ni kwa kurejea taaluma hiyo, anafuatilia mafanikio na haja ya kuwa na safu inayobeba dira na nguvu kufanikisha madeni yake manne, yaliyoorodheshwa kufanikisha malengo ya nchi.

Kama ilivyo chombo chochote kikubwa na kizito ikiwamo serikali, namna ya utendaji huwa kunajitokeza pengo la umri mkubwa wenye darasa, ndio hapo wanapoonenana kina- Lukuvi na Prof. Kabudi.

Watu wazima ni kada waliokusanya elimu ya asili, darasa na uzoefu na wana ufunguo wa kupenya pengi. Hilo si geni, kwani Rais aliwekeza hata katika mifumo ya utendaji wake kichama hivi karibuni katika Sekretarieti ya CCM, alipowakabidhi wakongwe na wasomi, waliongia katika chama ni wanafunzi, leo 'umri wao unasoma miaka 50...' na vishangilio 'Dk.' Na wengine wahitimu wa uhasibu ngazi za juu nchini (CPA).

Hata kabla ya hapo, ndio sababu ya Mtendaji Mkuu wa Kwanza CCM kuwa Mzee Pius Msekwa, akiwa na uzoefu kuongoza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, akamuachia Mzee Rashid Kawawa, hata baadaye wakaonekana Philip Mangula, Abdulharaman Kinana, na Yusuph Makamba.

Vyote hivyo vinaangukia katika dhana uwekezaji warasilimalwatu katika mfumo wa utendaji, kuzalisha zao bora la utendaji katika mfumo unaokusudiwa kutenda. Ni aina ya uwekezaji unaotumika sana katika vyuo vikuu na nyumba za ibada, kutokana na majukumu mazito walio nayo kwa jamii.

Nadharia hiyo ya uwekezaji, ndio Rais Dk. Samia amekuwa wakati wote yu makini nayo, ikichukua msingi wa kuteua na 'kutumbua' asiyefaa katika nafasi mbalimbali.

Hata inapochimbwa historia ya nchi baada ya uhuru, moja ya hatua za awali za uongozi wa Rais Nyerere, katika kufanikisha mageuzi hayo ya uwekezaji katika nguvukazi, alitanua elimu iwafikie Watanzania wengi, huku akiwapa nafasi zaidi za utendaji kuziba walizokuwa nazo wageni na ndio kuanza kujengwa shule za msingi kwa kasi nchini hali kadhalika vyuo ikiwamo IDM Mzumbe.

Pia, akaomba fursa kama hizo nje ya mipaka kaa mataifa marafiki, wengi wakienda shule katika nchi kama China, Iliyokuwa Jamhuri ya Muungano ya Urusi (USSR), hasa kundi kubwa likaangukia Chuo Kikuu cha Lumumba, kilichopokea wengi kutoka Afrika, vilevile vyuo vya Uingereza .

Nyumbani programu mbalimbali za mafunzo zilibukiwa, ikiwamo za kilimo, afya, ulinzi na siasa na hata ilipofika mwazoni mwa miaka ya 1970, ikiwa ni sehemu ya kutekeleza Azimio la Arusha, chama tawala wakati huo TANU, ikapitisha iliyojulikana Azimio la Musoma, lillikwa mahsusi katika elimu, ukibaki msingi a mzizi wa kunusuru wasiopata elimu kutokana na madhila ya ukoloni na nchi kwa 'Kisomo Chenye Manufaa.'


Mradi wa aina hiyo ukashuhudiwa duniani katika mataifa machanga, kuwekezwa katika rasilimaliwaatu duniani, kupitia shirika la Umoja wa Mataifa mahsusi kwa elimu na sayansi - UNESCO.

Pia, nchini kulishudiwa wataalamu wengi kuwanoa Watanzania, ikiwamo kwenye Ulinzi na Usalama, Kilimo na Elimu. Haikushangaza hadi kufika katikati ya miaka 1970, Umoja wa Mataifa ukaitaja Tanzania imefanikiwa kuwekeza kwa mafanikio hasa eneo la 'Elimu ya Awali' kwa maana kusoma na kujandika hadi kwa watu wazima waliokosa fursa.

Katika historia hiyo, imeendelezwa na awamu zote za uongozi, leo hii msomi wa uchumi, pia utawala wa umma na rasilimaliwatu, Rais Dk. Samia, akiendeleza mahitaji yake ya leo.

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# 'Goli la Mama' tamu lakini chungu






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

WANASEMA pesa ni sabuni ya roho. Na wanaosema hivyo ni waliozaliwa katika karne za hivi karibuni, baada ya mapinduzi ya viwanda huko Ulaya! Mapinduzi hayo tumekuwa tukifundishwa kwenye Historia shuleni.

Kwamba bila mabadiliko hayo kufanyika Ughaibuni, bila shaka tungeendelea kuishi kwa kufanya biashara ya kubadilishana mali na si kuuziana kwa sarafu na noti kama ilivyo hivi sasa.

Kama hamkumbuki, basi jueni kuwa zamani tulibadilishana chakula na bidhaa zingine, kama ulikuwa na mtama mimi jembe, ukanipa gunia moja au hata mkuki ulinipa debe la muhogo aka udaga au makopa.

Mapinduzi yakaleta sarafu na noti, na hivi sasa mwenye sarafu au noti ndiye anaheshimika katika jamii. Na kwa ujinga wetu, hata mwenye ng'ombe 100 anaonekana si mali kitu mbele ya mwenye Sh milioni tano!

Fedha tumeipa hadhi kuliko hata hadhi ya binadamu. Unaweza kusikia mtu anasema "nitakupiga nikuue, nikulipe." Atalipa nini? Fedha! Anadhani thamani ya utu ni sarafu na noti. Mwenye fedha akaitwa tajiri na kufunika mwenye watoto!

Leo mitaani, kuna vijana wanatamba kuwa na fedha, wanaonekana wakizianika kama si kwenye magari bali mifukoni na kwenye mabegi yao na kupita nazo barabarani kuzuga wasionazo.

Tunashuhudia mitandaoni vijana wakitamba, ukisikia mimi ni kijana mdogo tajiri mwenye fedha na hata kutukana wasionazo kuwa "we mpumbavu unayetazama video hii njoo nikufundishwe jinsi ya kupata fedha!"

Tunashuhudia matajiri mijini wakimiliki mali na hata watu kwa majina ya timu za soka na kupewa vyeo vya wafadhili au wadhamini, kutokana na ukwasi walionao.

Wengine tunawaona kwenye mikusanyiko ya sherehe, hususan harusi wakipita mbele kutuza maharusi, huku wakitapanya fedha sakafuni wakizikanyaga na kushangiliwa na wahudhuriaji kwa kuwaita 'Tajiri! Tajiri!', ilimradi wakiwavimbisha vichwa vyana kuzimwaga zaidi.

Juzikati hapa ndugu zangu Mwanza walishuhudia kufuru kama hii, na punde Jeshi la Polisi likawatuliza waliokuwa wakitupa fedha sakafuni na kuwaweka kunakohusika kwa tuhuma za kutoheshimu amana hiyo ya kiuchumi.

Bila shaka wahusika hawajatoa somo la kutosha kuhusu tabia hii ya kurusha na kutupa fedha sakafuni, au kufikicha fedha na kuzificha sehemu za siri kwa baadhi ya watu, lakini pia kuzishika huku mikono ikiwa michafu kama ya 'Paulo'.

Pengine hatua iliyochukuliwa na dogo Wilbrod Mutafungwa wa Mwanza kwa jamaa zangu wale akina 'getegete', litakuwa onyo na funzo kwa wenye nia ya kufanya hivyo, ili kujipatia ujiko kwenye mikusanyiko kama ule.Lakini pia, pengine hatua kama hiyo inapaswa kuchukuliwa hata kwa wanaojianika na mabulungutu ya noti barabarani au mitandaoni na kutambia wengine, kana kwamba kufanya hivyo kunaongeza tija, au kama si tu kujitangaza kuzipata kwa njia zisizoeleweka.

Serikali inapohimiza watu kuhifadhi fedha zao benki, si kwamba inawahurumia saana wanapokaa nazo majumbani, kuwa labda zinaweza kuibwa au kuungua au kukumbwa na ajali nyingine, ah ah, inataka zizungushwe na kuchangia kwenye uchumi.

Hivyo, kukaa nazo majumbani au kwenye magari ili kuringishia si sawa kabisa, nao wa hivyo hata kama ni wanachama wa 'Friimasoni', waelekezwe la kufanya na kuhakikisha ujinga wanaofanya haurudii.

Na ndiyo maana pia, nachukua fursa hii kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuja na ubunifu wa 'Goli la Mama' katika michuano ya kimataifa ya klabu za soka za wanaume, ambako amekuwa akinunua kila goli linalofungwa na klabu ya nchini inapocheza na ya ugenini na kushinda.

Lakini natilia shaka jinsi fedha hizo zinavyotolewa, pale ambapo mtoaji hulazimika kusafiri na bulungutu la noti na kukaa nalo uwanjani, sijui kwa usalama upi, na kuja kutoa mwishoni mshindi anapokuwa amepatikana kwa idadi ya magoli fulani yasiyotabiriwa.

Hebu fikiria, kwanza huwa haijulikani mshindi atafunga mangapi. Ina maana fedha huletwa zikiwa hazijui kuwa zitarudi au zitabaki zote. Na ni kiasi gani? Mathalan yakifungwa 10, atakuwa na kiasi gani uwanjani?

Kama makombe huandikwa nani kashinda na kutwaa palepale uwanjani baada ya mechi, kwa nini mleta fedha asije na hundi bandia na kalamu akaandika kiasi cha fedha na mshindi na kukabidhi hundi na fedha kuingizwa kwenye akaunti ya mshindi? Nini kitaharibika? Tujaribu tuone.

BIASHARA

# Ndivyo kutokurasimisha biashara zao kunavyowaweka kando kimafanikio

**Na Restuta James**

BIASHARA nyingi hasa za wanawake, hazikidhi baadhi ya matakwa ya kisheria kama kuzisajili, ambayo kama yangezingatiwa, yangewafungulia fursa ya masoko makubwa ya ndani na nje.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, anasema changamoto inayokabili biashara za wanawake, vijana na wenye ulemavu ni kutorasimishwa, hivyo kukosa fursa ya kupata zabuni.

Anasema sheria ya ununuzi inazitaka mamlaka zote za nchi kuanzia serikali kuu, kutenga asilimia 30 ya bajeti yake ya ununuzi, kwa ajili ya kampuni za wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu.

"Kama tutazipata zikaingia kwenye biashara zetu zitachochea sana ukuaji wa uchumi wenye matokeo makubwa. Nataka niwape hiyo changamato wanawake, vijana na watu wenye ulemavu pamoja na wazee kwamba turasimishe biashara zetu ili tuweze kuteka hizi fursa," anasema.

Anasema makundi hayo yanapaswa kuzingatia utunzaji wa kumbukumbu za biashara, ubora, kuwa na uwezo wa kutoa huduma baada ya makubaliano na kutumia teknolojia kuingia kwenye mifumo ya kuomba zabuni.

"Zabuni inaweza kukuambia upeleke kiasi fulani kila wiki au mwezi na usiishiwe. Tukiweza kufanikiwa kwenye ubora na uwezo wa kulishika soko, tutaweza kuingia kwenye masoko ya ndani na ya nje," anasema.

Ili kumudu zabuni kubwa, anashauri kampuni ndogo kuungana kwa lengo la kuzalisha kwa wingi na kwa ubora unaotakiwa.



Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) Bengi'i Issa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Chemba ya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC), kwa kuangalia upungufu huo wa masuala ya kisheria kwenye miradi ya wanawake, kwa kuanzisha programu maalumu ya kuwaelimisha wanawake na vijana namna ya kupata zabuni za umma.

Programu hiyo 'Bid for success' ikifupishwa B4S, inataka kuona asilimia 30 ya bajeti ya ununuzi wa umma inayokadiriwa kuwa zaidi ya Sh. trilioni mbili mwaka huu wa fedha 2024/25, inaingia kwenye kampuni zinazomilikiwa na wanawake pamoja na vijana.

Mwajuma Hamza ni Mkurugenzi Mtendaji wa TWCC, anayeeleza kuwa utafiti wa chemba hiyo wa mwaka 2021, ulibaini kwamba wanawake, vijana na makundi maalumu yanayoshinda zabuni za serikali ni chini ya asilimia mbili.

Anasema utafiti ulifanikisha mabadiliko ya sheria na kutungwa kwa kanuni zinazoelekeza ushiriki wa kila kundi kwenye zabuni za umma ili fedha hizo ziingie kwenye 'mifuko' ya makundi hayo maalum.

"Tukasema soko la serikali ni kubwa, bajeti ya mwaka huu wa fedha ni Sh. trilioni 49.3 ambazo asilimia 70 inakwenda kwenye ununuzi. Miradi mikubwa inatekelezwa, sisi wanawake ni lazima tushiriki kwenye fursa hizi, vinginevyo tutakuwa watazamaji," anasema.

Anasema B4S inalenga kuwapa wanawake na vijana taarifa za masoko na zabuni za umma, namna ya kuomba na kutimiza makubaliano.

"Tunalenga kuwajengea uwezo wanawake na vijana ili wakashindane kwenye zabuni na kuonyesha matokeo. Tunataka kuona ongezeko la wanawake kutumia hii fursa. Kwa mfano, wakati fulani, Wizara ya Ujenzi ilitangaza zabuni ambayo ilitenga Sh. bilioni 80 kwa ajili ya kampuni za wanawake, ni wanawake sita tu ndio waliomba...hii inatupa picha kwamba bado tuna kazi kubwa ya kufanya," anasema.

"Wakati tunahamasisha na kuhakikisha ofisi za umma zinatenga asilimia 30 kwa ajili ya makundi haya, sisi tuhakikishe wanawake wana uwezo...serikali inaweza kutenga halafu watu wakawa hawana uwezo wa kuzitumia hizi fursa, hatuwezi kwenda mbele," anasema.

Mkurugenzi Mkazi wa Trade Mark Afrika, Elibariki Shammy, anasema utafiti wa mwaka 2021, ulibaini kwamba baadhi ya watumishi wa Halmashauri na idara za serikali, hawakuwa na uwezo wa kuandaa zabuni inayokidhi uwezo wa kampuni zinazomilikiwa na makundi maalumu.

"Kuna suala la kujenga uwezo na kushirikiana ili zile zabuni zinapoandaliwa, zikidhi mahitaji ya kampuni za makundi haya. Kwenye zabuni ni utaalamu wa kuandika kile kinachohitajika na ushindani wa bei. Walaji wanapochagua bidhaa hawazingatii mzalishaji bali ubora na bei," anasema.

Anasema: "Masoko siyo shida, tuna hii asilimia 30 ambayo pia hatujaweza kuitumia...bidhaa za Afrika haziuzi sana sokoni kwa sababu ya ubora, bei na uwezo wa kuhudumia soko kwa muda mrefu."

Anatahadhalirisha kwamba kuomba zabuni ya umma na kushinda ni hatua moja na kulipwa baada ya kutimiza makubaliano ni hatua nyingine.

"Kama tunahitaji kutengeneza uchumi ambao unawalenga wanawake, vijana na makundi maalumu ni muhimu kutazama kwa upana sera na taratibu za biashara ili kuwezesha ukuaji wa uchumi unaowagusa wananchi wengi," anasema Shammy.

"Serikali inapaswa kuwa na sera madhubuti ya kukuza viwanda vya ndani ili wazawa wanaposhinda zabuni, mzunguko wa fedha ubakie kwenye uchumi nchini. Isipowalipa kwa wakati, kampuni hizi zitakufa mapema na lengo la kuwainua halitafikiwa," anasema.

Anasema ni muhimu kutengeneza bishara endelevu na hasa viwanda ili kubakisha fedha ndani ya nchi, badala ya kuagiza nje.

"Ili viwanda viwepo ni muhimu sera zizungumze vizuri na mahitaji ya nchi katika maeneo mbalimbali ili kuzalisha ajira na kuondoa umasikini. Hakuna nchi isiyokuwa na utaratibu, lakini usipokuwa rafiki kila mtu anapoteza," anasema.

Ofisa Mwandamizi katika Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Elias Chaponde, anasema sheria ya PPRA sura na 410 ya mwaka 2023 kifungu cha 64, inazielekeza Halmashauri na ofisi zote za serikali kutenga bajeti yake ya ununuzi kila mwaka kwa ajili ya wazabuni wanawake, vijana na makundi maalumu.

Anasema kanuni za sheria hiyo (PPR), ambazo zimeanza kutumia mwaka huu wa fedha 2024/2025, zinazitaka ofisi za umma kutenga asilimia 30 ya bajeti ya ununuzi kwa ajili ya makundi hayo.

"PPRA kazi yake ni kufuatilia na kusimamia kuhakikisha kwamba taasisi za umma zinatekeleza takwa hilo la kisheria kwa kutenga hiyo asilimia 30 kwa ajili ya wanawake, vijana na makundi maalumu na kutoa ripoti," anasema.

## DODOMA KUWA SHULE YA KILIMO, DARASA LIKIELIMISHA WAKATI WOTE

Inatoka Uk 11

heni elimu ya kila mkulima alichotaka.

Mkazi wa Manyoni, Andrew Peter, anajivunia kupata elimu kuhusu mbegu bora za mazao na jinsi ya kutumia mbolea kwa ufanisi kuondokana na kilimo cha mazoea.

Anazungumzia vifaa vya kisasa vya kilimo ambavyo vitabadilisha uzalishaji shambani na kuongeza tija.

Pendo Mahikwi anasema maonesho ya mwaka huu yamekuwa ni ya tofauti yakiwawezesha kujifunza zaidi tofauti na ya awali walikuwa wakiishia kuyaona ni eneo la kwenda kutembea na kununua bidhaa mbalimbali.

"Tumepata nafasi ya kujifunza teknolojia mpya za kilimo kama matumizi ya mbegu zinazostahimili ukame. Hii itatuongezea mavuno na kupunguza hasara tunazopata kutokana na mabadiliko ya tabianchi,"anasema.

Mfugaji kuku, Alfonsina Mahindoni, anasema Nanenane imempa maarifa mapya kuhusu lishe bora ya kuku na jinsi ya kupunguza magonjwa.

**MAHARAGE MAPYA**

Mtafiti wa magonjwa ya mimea kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kituo cha Selian, Edith Kadege anasema Nanenane imetoa elimu kwa wananchi kuhusu mbegu mpya za maharage yenye ukinzani na magonjwa ya baka pembe, chule na kutu ya majani.

"Tumewaelimisha wakulima kutumia mbegu hizo mavuno yataongezeka hadi kufikia magunia sita mpaka nane yenye kilo 100 kwa ekari na yenye madini ya kutosha,"anasema.

Maonesho ya Nanenane hutoa fursa kwa wananchi kujifunza teknolojia mpya, mbinu bora za kilimo na masoko ya bidhaa kuongeza kipato chao na taifa.





## Wananchi watakakiwa kuchangamkia kujisajili NeST

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA) imewataka wananchi kujisajili na Mfumo wa Usimamizi wa Ununuzi wa Umma Kielektroniki (NeST) ili wapate fursa ya kufanya biashara kupitia zabuni zinazotolewa na serikali.

Mkurugenzi Mkuu wa PPRA, Denis Simba, alitoa rai hiyo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya uzinduzi wa mfumo huo, utakaofanya mwezi ujao na Rais Samia Suluhu Hassan jijini Arusha.

"Wizara ya Fedha kupitia PPRA inaandaa Kongamano la 16 la Ununuzi wa Umma la Afrika Mashariki, litakalofanyika Septemba 9 hadi 12, mwaka huu, jijini Arusha, ambapo nchi zaidi ya nane zinakutana Arusha kujadili kuhusu matumizi ya dijitali kwenye sekta ya ununuzi wa umma," alisema

Alisema katika tukio hilo, Rais Samia atafungua kongamano hilo na kuzindua rasmi NeST.

"Tungependa Watanzania wafahamu kuwa zaidi ya asilimia 70 ya Bajeti ya Serikali inatumika kupitia tenda za serikali kwa lugha rasmi ni ununuzi wa umma. Sasa tenda zote zimewekwa kiganjani kwa kila Mtanzania kupitia tovuti ya nest.go.tz.

"Kwahiyo, kila Mtanzania anaweza kuziona tenda za serikali, kushiriki kuomba akiwa na vigezo, na mwenye vigezo zaidi atapata tenda kwa haki, usawa na kwa uwazi," alisisitiza

Alisema mtu anapaswa kujisajili kupitia mfumo huo ili afanye biashara na serikali na kuongeza ajira na vipato kwani fursa hiyo sasa ni ya watu wote.

"Niwaambie tu kuna fursa kubwa kwenye michezo kupitia tenda za serikali, ambazo zipo kwenye Mfumo wa NeST kwa mfano, Mzabuni anayejenga Uwanja wa Mpira wa Miguu jijini Arusha utakaotumika kwenye michuano ya AFCON 2027 (Samia Stadium), amepatikana kupitia Mfumo wa NeST."alisema

Alisema ujenzi huo utakaogharimu zaidi ya Sh. bilioni 286, utatoa ajira nyingi kwa Watanzania.

"Vivyo hivyo, kwa ukarabati na ujenzi wa viwanja vya serikali, PPRA wanafuatilia upatikanaji wa wazabuni hadi utekelezaji wa mikataba yake," alisema.

# Dk. Mpango kuzindua wiki ya usalama barabarani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Phillip Mpango anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani kitaifa jijini hapa jumatatu ijayo.

Hayo yalisemwa na Naibu Kamishna wa Jeshi la Polisi mstaafu, Mohammed Mpinga wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusiana na maadhimisho ya wiki hiyo na Miaka 50 ya Baraza la Usalama Barabarani nchini yatakayofanyika katika Uwanja wa Jamhuri jijini hapa.

Mpinga, alisema katika maadhimisho hayo pamoja na mambo mengine utazinduliwa mkakati wa kukabiliana na ajali nchini.

"Mwaka huu pamoja na Maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama barabarani, pia ni Maadhimisho ya Miaka 50 ya Baraza la Taifa la Usalama barabarani, hivyo mkakati mwingine wa kukabiliana na ajali utazinduliwa kwa ajili ya miaka mingine 50," alisema.

Alizitaja shughuli zitakazofanyika katika wiki hiyo kuwa ni pamoja na utoaji elimu kwa wananchi juu ya masuala ya usalama barabarani.

Hata hivyo, alisema jukumu la usalama barabarani ni la kila mwananchi, hivyo wanapswa kujitokeza ili kupata elimu kuhusu masuala ya usalama barabarani.

Awali Mkuu wa Kikosi cha Usalama barabarani nchini, Ramadhan Ng'azi aliwataka wamiliki wa vyombo vya moto kuvipeleka kufanyika ukaguzi kuanzia jumatatu ijayo.

Ng'azi alisema kuwa vyombo vya moto ambavyo havitafanyiwa ukaguzi havitaruhusiwa kutembea barabarani hadi vikaguliwe na kupatiwa stika.

"Chombo ambacho kitakamatwa barabarani kikiwa hakijakaguliwa kitakamatwa na kupelekwa polisi kwa ajili ya ukaguzi na kama kitakaguliwa na kukutwa kikiwa bado na matatizo hakitarudishwa hadi kionekane kuwa kipo sawa kwa ajili ya matumizi ya barabara zetu," alisema.

Ng'azi, aliwataka wamiliki wa vyombo hivyo nchini kutumia kipindi hicho kupeleka magari yao kukaguliwa kwa hiyari na kupatiwa stika kuonyesha kiko salama kutembea barabarani.

"Nitoe wito kwa wamiliki wa vyombo vya moto nchini kutumia kipindi hiki kilichobaki kufanya ukaguzi wa vyombo vyao ili kuepuka usumbufu wa kukamatwa na jeshi la polisi wakati wa ukaguzi," alisema

Akizungumzia kuhusu mabasi yanayotembea usiku, alisema kikosi hicho kimeweka mikakati ya kuzuia ajali, ikiwemo kupima kiwango cha ulevi cha madereva.

Alitaja mikakati mingine kuwa ni kuhakikisha wanafunga vifaa vya kudhibiti mwendo kasi na mabasi yanayosafiri umbali mrefu kuwa na madereva wawili.




Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, DCP Ramadhan Ng'azi, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma juzi, kuhusu maadhimisho ya wiki ya nenda kwa usalama barabarani na maadhimisho ya miaka 50 ya Baraza la Taifa la Usalama Barabarani yanayotarajiwa kufanyika Agosti 26 mwaka huu, mkoani humo. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Madalali wadaiwa kuwalaghai wakulima wa dengu

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

WAKULIMA wa dengu katika Halmashauri ya Itigi wilayani Manyoni Mkoa wa Singida wameiomba serikali kuwapa elimu ya mfumo wa stakabadhi gharani kufanya biashara kwa mnada na kuondokana na udanganyifu wanaodai kufanyiwa baadhi ya madalali mashambani.

Wakizungumza na waandishi wa habari juzi kwa nyakati tofauti, walisema wametoa ombi hilo baada ya kubaini kuwa madalali wanaofika vijijini wanawapotosha kuhusu mfumo huo kwa lengo la kuwalangua mazao yao.

Walisema madalali hao wamekuwa wakiwaeleza kuwa wakipeleka mazao yao kuuza kwa mfumo huo watadhulumiwa fedha zao.

Walisema madalali hao wamekuwa wakiwaambia kwamba kwa mfumo huo, huenda ikachukua hata miaka mitatu zaidi kulipwa fedha zao.

Wakulima hao ambao walikuwa wakizungumza m katika ghara la Utemini Itigi linalotumika kukusanya na kuuzia dengu kwa njia ya stakabadhi gharani, walisema madalali wanaopita mtaani wananunua kwa bei kati ya Sh.1,300 hadi Sh.1,500 kwa kilo.

Walisema wasimamizi wa mfumo huo nao wamekuwa wakisema kwa minada mitatu iliofanyika mpaka sasa bei ya zao hilo haijashuka chini ya Sh. 1,900.

Fidelis Mtoka, mkulima wa Kijiji cha Kazikazi Kata ya Kitalaka, alisema mpaka bado hajapata elimu ya kutosha juu ya mfumo huo na kubaki njia panda.

"Kwangu bado mfumo sijauelewa vizuri, changamoto kubwa inayotupata sisi wakulima ni kuhusu bei, elimu haijatufikia," alisema.

Mkulima mwingine, Issa Abdalla, aliitaka serikali iwape elimu wakulima hususani vijijini ili waondokane na kauli za udanganyifu zinazotolewa na madalali hao.

"Siku ya kwanza nilipoambiwa kuhusu kupeleka mazao gharani nilipingana nao sana sababu sikuwa na elimu kuhusu mfumo ila baada ya kufuatilia nilielewa na nikajiunga," alisema.

Abdallah, alisema hakuamini kama mfumo huo utakuwa kama anavyoshuhudia licha kuishauri serikali iwafikie zaidi wakulima hasa waishio nje ya mji.

Mwendesha ghala kuu kwa mfumo huo wa halmashauri ya Itigi na Manyoni, Remigeous Kailembo, alisema kadiri siku zinavyokwenda wakulima wanajitokeza zaidi kupeleka mazao yao gharani.

Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika na Masoko (AMCOS) Utemini Itigi, Geofrey Yohana, alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wakulima kwa kutumia magari kwa wakulima.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo ya Itigi, Jonathan Dulle, alisema kama halmashauri mpaka sasa wamekusanya zaidi ya Sh. milioni 160 katika minada mitatu mwaka huu na hawajapokea malalamiko ya mkulima kutopokea hela ndani ya saa 48.



# Ndugu wawili wafariki dunia wakifukiwa na kifusi mgodini

**Na Elizabeth John,**
WANGING'OMBE

NDUGU wa familia moja, Okoka Mkaleja (24) na Yusuph Mkaleja (21) wa Kijiji cha Kiumba Halmashauri ya Mji wa Makambako wamefariki dunia kwa kuporomokewa na mawe wakati wakichimba madini.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi Mohamoud Banga amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema ndugu hao walikuwa wachimba madini aina ya ulanga katika mgodi unaomilikiwa na Willson Manongi.

Kamanda Banga alisema tukio hilo lilitokea Agosti 21 majira ya saa tano na nusu asubuhi katika Kijiji cha Ulanga.

"Kwahiyo wakati wanaendelea kuchimba madini ndipo kifusi kikawaangukia, pale wapo wachimbaji wengine wengi lakini walioingia ilikuwa ni hao wawili," alisema Banga.

Hivyo, alitoa wito kwa wamiliki wa migodi kwamba machimbo yanapaswa kujengewa ili kuzuia udongo usiporomoke na kuleta athari ikiwemo vifo.

Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Claudia Kitta alisema ndugu hao walitangulia mgodini hapo na baadaye walimuita baba yao kuchimba.

"Kwa hiyo baba yao ameshuhudia tukio hili la watoto wake wawili, kwa hiyo tumepeleka miili hiyo Hospitali ya Ikelu ambayo ipo karibu na Makambako ili iwe rahisi kwa mazishi," alisema Kitta.

Kitta alisema vijana hao hawakuwa na vifaa vya usalama ikiwemo kofia ngumu na hata walivyopewa tahadhari hawakuzingatia.

Alisema: "Waliwahi kuambiwa kwamba eneo hilo linaonekana kama lina hatari kwa hiyo wasiingie lakini kwa kuwa madini hayo yanachimbwa na yanauzwa kwa kadri ulivyochimba mengi basi wakawa hawajasikia hiyo tahadhari waliyopewa".

Alisema walichukua hatua ya kwenda eneo la tukio na kubaini kwamba kampuni ya uchimbaji madini inayo leseni na inatambulika.



Wapigadebe kutoka Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli, Dar es Salaam, wakiwa wamezingira daladala katika kituo cha Mbezi Mwisho, wakijiandaa kugombea abiria waliofika hapo, kwa ajili ya kusafiri, kitendo kinachosababisha usumbufu mkubwa juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mawakala pembejeo waomba kujumuishwa bei ya usafiri

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MAWAKALA wa pembejeo za kilimo Makambako mkoani Njombe wameiomba serikali kuongeza bei ya usafirishaji wa mbolea ya ruzuku inayokwenda maeneo ya vijijini, ili ziwafikie wakulima kwa wakati na kwa gharama nafuu.

Walitoa ombi hilo baada ya serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kutangaza bei elekezi za mbolea katika msimu wa kilimo wa mwaka 2024/2025.

Wakizungumza katika kikao kilichowakutanisha wadau wa kilimo hasa kampuni za mbolea, mbegu, mawakala na wakulima wa mkoani Njombe ambacho kimefanyika ukumbi wa Lutheran Center mijini Makambako walisema bei za msimu uliopita hazikuwa na uhalisia.

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa pembejeo za kilimo Mkoa wa Njombe, Abusalum Magoma alisema kutokana na bei kutokuwa na uhalisia ziliwalazimu baadhi yao hasa wanaopeleka mbolea vijijini kuongeza bei kutokana na gharama za usafirisha na kuonekana wanaihujumu serikali.

Seth Vegulla aliiomba serikali kuja na majibu ya haraka ikiwa itaweka bei elekezi kwenye mbegu ili kuwawezesha muda wa kuzipata mbegu hizo.

Bwana shamba wa kampuni ya OCP, Joshua Joely alisema watahakikksha mbolea zinawafikia wakulima kwa wakati, huku wakitaka wakulima kutoa taarifa pindi wanapouziwa mbolea ujazo tofauti na kilo 50.

Baadhi ya wakulima wa Halmashauri ya Makambako akiwemo Thomson Nziku aliitaka serikali kukabiliana na wakala wanaowauzia mbegu feki na wale wanaopunguza ujazo wa mbolea.

Ofisa Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Betrice Tarimo aliwataka mawakala wa pembejeo za kilimo kuzingatia bei elekezi ya mbolea ambayo imetolewa na serikali.

Pia aliwataka wakulima kuendelea kujisajili katika vijiji vyao ili wanufaike na mbolea ya ruzuku.

# Jafo: Tanzania yaupiga mwingi utekelezaji SDGs

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, amesema Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizofanya vizuri katika utekelezaji wa Malengo Endelevu ya Milenia (SDGs) ikiwemo lengo namba tatu na la sita.

Alisema hayo juzi wakati akipokea taarifa ya mradi wa uboreshaji wa tabia za usafi kwenye shule 30 na vituo vya afya 15 katika Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani.

Mradi huo umegharimu zaidi ya Sh. bilioni nne, umefadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) kwa kushirikiana na Shirika la WaterAid.

Alisema lengo la tatu linalenga kuhakikisha maisha ya watu wenye afya njema na ustawi wa watu wote wa rika.

Jafo alisema lengo la sita linalohusu upatikanaji wa maji salama, usafi wa mazingira na usafi kama hitaji la msingi zaidi la afya na ustawi wa binadamu yamefanikiwa.

Alisema katika malengo hayo mawili WaterAid na JICA imesaidia jitihada za serikali kufikia malengo waliyokusudia na wananchi kupata maendeleo.

Aidha, alisema kuboreshwa kwa huduma za maji, usafi wa mazingira katika Wilaya ya Kisarawe kutasaidia ukuaji wa uchumi na kupunguza magonjwa yatokananyo na kukosekana kwa huduma ya maji.

Jafo alisema: "Fedha nyingi zinapotea kitibu magonjwa yanayosababishwa na maji, hivyo kupatikana kwa maji safi kunapunguza tatizo hilo na watu kukua kiuchumi na kuikinga jamii na magonjwa yatokanayo na hali duni ya usafi".

Mkurugenzi Mkaazi wa Shirika la WaterAid, Ana Mzinga, alisema kwa ufadhili wa Shirika la JICA waliweza kubuni mradi wa kufundisha namna bora ya matumizi ya maji katika vituo vya afya 15 na shule 30 wilayani Kisarawe.

Alisema mradi huo wameufanya katika kipindi cha miaka mitatu, wamepata ushirikiano kutoka serikalini na wadau wa maendeleo ambao wamesaidia kufanikisha utafiti huo.

Mzinga alisema katika utafiti huo waligundua utumiaji wa maji hasa baada ya kutoka chooni ulikuwa upo chini kutokana na uelewa na ukosefu wa miundombinu ya kuwawezesha kunawa mikono kwa wanafunzi wanapotumia vyoo.

Alisema walianza kuboresha miundombinu ili kuhakikisha maji yanapatikana katika shule na vituo vya afya pamoja na kutoa elimu iliyowawezesha kujua ni wakati gani wanatakiwa kunawa mikono wanapotumia choo.

Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Petro Magoti, alisema wilaya hiyo bado inahitaji msaada huo zaidi kwani utasaidia kuwaepusha watoto na magonjwa yatokanayo na maji, hivyo kuboresha ufaulu wao.

Alisema: "Kisarawe kuna matukio mengi ya ukatili wa kijinsia, tukimsaidia mtoto wa kike akapata maji safi na salama kwa urahisi tutakuwa tumeikoa wilaya yetu, hivyo niwaombe WaterAid na JICA kuendelea kutusaidia hasa katika shule za mbali".

Tatibu wa Zahanati ya Kiurui, Launi Mwanyika, alisema mradi huo umewasaidia upatikanaji wa maji, wana uwezo wa kuyahifadhi kwa muda mrefu bila kuwa na changamoto ya huduma hiyo.



# Ajali za barabarani zapungua Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

AJALI za barabarani kwa kipindi cha Julai 2024 Zanzibar zimepungua na kufikia ajali 21, kutoka ajali 23 zilizoripotiwa Juni.

Ofisa Takwimu kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Ahmada Hassan Suleiman alitoa takwimu hizo juzi wakati akiwasilisha taarifa za matukio hayo visiwani Zanzibar.

Alisema kati ya matukio hayo, Wilaya ya Magharibi A Unguja imeripoti matukio zaidi ya Matano, Wilaya ya Kati Unguja (4).

Alisema idadi ya ajali za barabarani kwa mwaka zimepungua kwa asilimia 12.5 na kufikia 21 kwa kipindi cha Julai 2024, kutoka ajali 24 kipindi cha Julai 2023.

Alisema Wilaya ya Magharibi A imeripotiwa kuwa na ajali tano na Julai 2023 Wilaya ya Micheweni ilikuwa na ajali tano.

Ahmada alisema katika ajali hizo waliofariki kwa kipindi cha Julai 2024 walikuwa idadi sawa na kipindi cha Juni 2024 ambao ni 17.

Alisema majeruhi wamepungua kwa asilimia 18.8 na kufikia 13 kwa kipindi cha Julai 2024 kutoka majeruhi 16 kipindi cha Juni 2024.

Alisema waathirika waliofariki kwa kipindi cha Julai 2024 waliongezeka kwa asilimia 6.3 hadi kufikia 17 kipindi cha Julai 2024 kutoka 16 walioripotiwa Julai 2023.

Kadhalika alisema kwa kipindi cha Julai 2024 waathirika wengi wa ajali ni abiria ambao walikuwa ni 12, huku waendesha baskeli na pikipiki tisa na watembea kwa miguu tisa.

Alisema makosa 5,436 yaliripotiwa kipindi cha Julai mwaka huu, kwamba makosa 5,424 yalikuwa ni wanaume na makosa 12 yalifanywa na wanawake.

# Dk. Mwinyi awatangazia neema wakulima mwani

**Na Mwandishi Wetu**

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema serikali inatarajia kuweka mkazo zaidi kwenye zao la mwani, ili kuzalisha bidhaa zenye ubora na kupata masoko ya uhakika.

Alisema hayo Ikulu, Zanzibar wakati akizungumza na Balozi wa Umoja wa Ulaya (EU) Tanzania, Christine Grau.

Alisema asilimia 99 ya wakulima wa mwani Zanzibar ni wanawake, hivyo alimweleza balozi huyo kuangalia namna ya kuwasaidia wanawake na wakulima wa mwani nchini hasa kutoa mafunzo na vifaa vya kisasa.

Kadhalika, Dk. Mwinyi alimweleza Balozi Grau kuwa uchumi wa bluu ni sera kuu ya uchumi wa Zanzibar, hivyo alimuomba kuangalia fursa zinazotokana na sera hiyo.

Naye Balozi Christine alisifu juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kueleza kuwa wanafanya kazi kwenye maeneo mbalimbali iliwemo kushirikiana na jamii kupitia serikali za mitaa na taasisi za kiraia.

Alisema kupitia mradi wao wa "Green City" wamesaidia masuala ya jinsia hasa kuwawezesha wanawake kwenye elimu, uchumi ikiwemo uvuvi, pamoja na masuala ya uongozi wa fedha.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza wakati wa Tamasha la Kizimkazi lililolenga kukuza Utalii Zanzibar, katika Uwanja wa Shekha Dimbani, juzi. **PICHA: OWM**

# Makamu wa Rais asisitiza uendelezaji utalii wa urithi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, amesema utalii wa urithi ni muhimu ukaendelezwa visiwani Zanzibar, kwa kuwa ndiyo unaongoza kuingiza fedha nyingi za kigeni, kukuza uchumi na ajira.

Alisema hayo Makunduchi katika shamrashamra za kuelekea kilele cha Tamasha la Kizimkazi, baada ya kuyapokea mashindano ya mbio za baiskeli zilizoanzia Unguja hadi Makunduchi kwa wanawake na watu wenye ulemavu.

Alisema Zanzibar inapiga hatua kubwa katika sekta ya maendeleo ya utalii kutokana na kuwepo utajiri mkubwa wa rasilimali za vivutio vingi vya urithi.

Alisema lakini urithi huo hauwezi kuwa na tija kubwa kama inavyotarajiwa iwapo wageni hawatokuja Zanzibar kuona alama hizo muhimu za urithi wa nchi zilizopo kihistoria.

Alisema ili kuurithisha kwa vizazi vya sasa ni vyema alama hizo za kihistoria kukumbushwa kwa kutangazwa kupitia masuala yanayowakusanya watu pamoja, ikiwemo kuandaa matamasha kama vile Kizimkazi.

Pia alisema miaka 100 iliyopita Zanzibar ilikuwa na idadi ndogo ya watu na kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 1910 idadi ya wakazi ilikuwa 100,097.

Alisema tamasha hilo ni muhimu katika kurithisha jamii na hasa vijana ili utalii na utamaduni uwe na faida na tija kubwa zaidi katika nchi.

Othman alisema matamasha kama hayo ni muhimu kuendelezwa kwa juhudi kubwa yatasaidia kukumbusha urithi uliopo na mambo mengine yanahusiana na masuala ya urithi na utamaduni nchini.

Alisema Mkoa wa Kusini una mambo mengi ya urithi likiwemo suala la tawala za jadi ambalo hata watawala waliokuja mwaka 1929 waliandika kitabu cha utamaduni wa watu wa Zanzibar na kuyafafanua mambo ya kiutamaduni.

Hivyo, aliwashauri waandaaji wa tamasha hilo kuyakumbusha mambo ya kiutamaduni ili kurejesha utamaduni wa kuwa na kumbukumbu za urithi.

Alisema ni vyema katika tamasha hilo kuweka siku maalumu ya wamalenga ili kusaidia kukuza na kuvilea vipaji vilivyopo vijana na kuonesha umahiri wa lugha ambao unaweza kusaidia kutunza na kuhifadhi utamaduni wa Wazanzibari ambao ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhani Soraga, alisema tamasha hilo ni fursa maalum kwa watu wa kusini kufungua zaidi sekta ya utalii, ambapo pia tamasha limetumika kutoa mafunzo kwa makundi mbalimbali yakiwemo wajasiriamali, wakulima, wafugaji na wasanii.

Alisema baadae mafunzo hayo waliyoyapata yatatumika kupima mafanikio katika mabadiliko ya kiuchumi kwa kila sekta iliyohusishwa.

Mudrik alisema ukuaji wa sekta hiyo ni muhimu katika kutoa fursa za ajira kwa vijana wa Zanzibar na kusaidia kupanua wigo zaidi kwa kufungua fursa.

Alisema kwamba pia jitihada hizo zinalenga kuifanya Zanzibar kuwa kituo muhimu cha utalii Afrika na duniani, kwamba ili kufanikiwa katika lengo na azma hiyo ni lazima juhudi maalum zielekezwe katika kuhifadhi mazingira ili Zanzibar ibaki kuwa kivutio kikubwa cha utalii.

Naye Mwenyekiti wa tamasha hilo, Mahfoudh Said Omar, alisema kwamba tamasha hilo linalenga kushirikisha makundi mengi zaidi ikiwa ni juhudi za pamoja za kukuza sekta mama ya utalii Zanzibar.

Alisema kwamba tamasha hilo ni la kimaendeleo, linalogusa kila aina ya watu ndani na nje ya Zanzibar ikiwa ni pamoja na kutumika fursa hiyo kuibua vipaji vya vijana kutoka maeneo mbalimbali vitakavyochangia jitihada za pamoja za kupunguza tatizo la ajira nchini.



Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (katikati), akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuendesha harambee ya kuchangisha fedha za ununuzi wa eneo la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Songambele, mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara juzi, ambapo Sh. milioni 53 zilipatikana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanasiasa walia gharama za matibabu

**Na Maulid Mmbaga**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Utetezi wa Umma (CHAUMMA), Kayumba Kaptali, amesema gharama za matibabu zimekuwa kubwa kwa Mtanzania wa kipato cha chini akiugua ni kama anachungulia kaburi.

Aidha, amesema ni vyema mamlaka ikaangalia kwa kuwa ni haki ya kila mwananchi kupata huduma bora ya afya.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati wa kongamano lililokutanisha baraza la vyama vya siasa Tanzania, kwa ajili ya kutoa maoni kuhusu Dira Mpya ya Maendeleo ya mwaka 2050.

Alisema wananchi wa kawaida wakiwamo wanaoishi vijijini wanasumbuliwa na gharama za vipimo vikubwa vya mionzi (MRI) na CT-Scan, ambavyo hutumika kufanya uchunguzi wa matibabu kwa kufanya tathmini ya majeraha, ufuatiliaji wa matibabu ya mgonjwa na mipango ya upasuaji.

"Ningependa kusisitiza kuwa ni muhimu sana hivi vitu viangaliwe kwasababu ni haki ya kila mtu kupata huduma ya afya kwakuwa ni jambo kubwa na la msingi katika taifa letu," alisema Kaptali.

Fatuma Seleman, aligusia suala la kinamama akidai kujifungua hospitali kumegeuzwa kuwa biashara yenye faida kubwa kutokana na gharama zilizowekwa katika vituo mbalimbali vya umma na binafsi.

Alisema gharama za kujifungua ni kubwa kote nchini na suala hilo linasababisha wanawake wengi kutoa mimba na kukimbiwa na waume zao kutokana na kuhofia gharama.

Pia, alisisitiza serikali kuangalia uwezekano wa kupunguza gharama hizo kwa wajawazito kwenye vituo na hospitali za umma na binafsi.

"Wazazi wa Tanzania wamekuwa ni biashara, mtu akipata mimba basi atafute mamilioni ya kwenda kujifungua, atafute nguo za kwenda kuzaa, amwambie mumewe atafute fedha za kwenda kule, kwakweli hiki kimekuwa kilio kikubwa vijijini mpaka mijini.

"Naomba serikali isikie kilio hiki, mwanamke apunguziwe gharama za uzazi, wanawake tumeachwa nyuma kwasababu ya kuzaa, tunakimbizwa na wanaume ukipata mimba mwanaume humpati tena, aliyekuweka anakukataa kama jambazi kwakuwa anaogopa gharama," alisema Fatuma.

Aidha, alidai kuwa kumekuwa na tatizo kubwa la baadhi ya wanawake kutoa mimba huko vijijini hasa wenye umri mdogo kwasababu ya kuogopa kiasi cha fedha atakacho toa, huku akisisitiza suala hilo lifikiriwe na kupewa kipaumbele ili wajifungue salama.

Baraza la Madiwani wa Manispaa ya Bukoba, waliitaka idara ya afya kuweka wazi gharama za vipimo, dawa, vifaa vya kujifungulia na huduma zote kwa wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano kwenye mbao za matangazo vituo vyote vya afya na zahanati.

Pia, baraza hilo lilitaka kujua sababu za wanawake kutozwa gharama mbalimbali wakati wa ujauzito, mahudhurio ya kiliniki pamoja na kununua dawa kabla au baada ya kujifungua, wakati sera na maagizo ya Wizara ya Afya yamekuwa yakisema huduma hizo ni bure.

Vile vile, ilielezwa kuwa licha ya maelekezo hayo ya sera, baadhi ya maeneo hukiukwa, na hospitali za umma na binafsi, wajawazito hutozwa gharama tofauti inayoanzia Sh. 200,000 na kuendelea kulingana na uhitaji wake wa matibabu ya ziada kutokana na matatizo mengine ya kiafya yanayomfika wakati wa kujifungua.

# CMA: Migogoro sehemu ya kazi ngumu kuepukika

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Divisheni ya Kazi, imesema migogoro ya kazi ni jambo ambalo si rahisi kuliepuka katika jamii yoyote inayoendelea kiuchumi.

Kwa kutambua hilo, imesema mahakama na wadau wana wajibu wa kuhakikisha wanakuwa na mifumo madhubuti ya kutatua migogoro hiyo.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Jaji Kiongozi, Mustapher Siyani wakati akifungua mkutano wa nane wa kamati ya utatu uliofanyika baina ya mahakama hiyo na wadau wa haki kazi.

Jaji Siyani aliwaeleza wadau wa haki kazi umuhimu wa mchakato na mabadiliko katika kuboresha huduma katika eneo la haki kazi na kuwataka kuwa tayari kupokea mabadiliko ili kuleta mapinduzi katika sekta ya kazi.

Pia Jaji Siyani alishauri wadau kuhakikisha wanakuwa na mifumo madhubuti na jumuishi inayosomana katika kutatua migogoro ya kazi nchini.

Alisema mfumo jumuishi ya kazi utasaidia kuweka urahisi wa michakato katika utatuzi wa migogoro kwa kuhakikisha haki za watu zinalindwa na migogoro kutatuliwa kwa wakati, pia kutakuwa na kushirikishana na kuwasaidia walalamikaji kuwasilisha malalamiko yao bila kuwa na vizuizi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Suzanne Doran alisema Mahakama Kuu imekwenda mbali zaidi kwenye masuala ya teknolojia na mfumo huo utakwenda kuboresha utoaji haki kwa wakati kwa kuwezesha wadau kuwasilisha mashauri yao kwa wakati.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), Usekelege Mpulla, alisema migogoro mingi ambayo wamekuwa wakipokea ni ya kuachishwa kazi au kuvunjwa kwa mikataba na kwa mwaka uliopita tume hiyo ilipokea migogoro 7,119 na asilimia 76 ya migogoro hiyo ilisuluhishwa kutokana na kurahishishwa mifumo ya utendaji kazi.


## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**JACKLINE BARNABAS MASSAWE** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria yenye namba **TAE662966** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 14/11/2023. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/173640/2024.**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo KAWE Wilaya ya KINONDONI**

**Kituo cha KAWE, Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la Madai/Ndoa Na 247...............2024**

**Jina la Mdai SERENE MICROFINANCE ( GRACE KWERU HR)**

**Jina la Mdaiwa ELIAMLISI JOSEPH MLAY**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: ELIAMLISI JOSEPH MLAY**
**WA MWENGE**
**DAR ES SALAAM**

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba
**FIKA HAPA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 28 mwezi 8 mwaka 2024 saa.........Asubuhi/Mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
Angalizo: kama hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini. Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe 19 mwezi 8 mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
KAWE



**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMNISTRATION CAUSE NO 17647 Of 2024**

**In the Matter of the Estate of the late ROSE HOSEA MAGALLA of KIKUYU within Dodoma Region**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY DAVID ANDREW HELLAR**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 27 Day of 08...................... 2024
Dated at Dodoma this 19 day of July.......... 2024

**PETITIONER**
**Presented for filing this 23 day of 7............2024**

RESIDENT MAGISTRATE



## KUPOTEA KWA CHETI



**EMANUEL JOHN PASTORY** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1190/0047** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **LUGUNGA SECONDARY** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/SHI/SHI/5069/2024.**



**FOMU MADAI - 3**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MASWA**

**Kituo cha NYALIKUNGU Mkoa wa SIMIYU**

**Shauri la Ndoa Na. 32/2024**

**Jina la mdai: JOYCE JAMES**

**Jina la mdaiwa: MANOJA LUSAKA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: MANOJA LUSAKA WA HINDUKI**
**K.K AFISA MTENDAJI KIJIJI CHA HINDUKI**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba
**ANADAI TALAKA ILI MUACHANE KWA KUWA UMEMTOROKA KWA MUDA MREFU**
Kwa hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 26 mwezi wa 08 Mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 19 Mwezi 08 Mwaka 2024.

MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU MASWA
HAKIMU
HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU



**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and administration Cause No 19549 of 2024**

**In the Matter of the late JONATHAN PETRO MAGAWA of Dodoma within Dodoma Region**

**And**

**In the Matter of an Application for letters of Administration by MAGRETH PETRO MAGAWA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 12 day of 09...................... 2024

**Dated at Dodoma this 13 day of 08................2024**

COURT SEAL DODOMA DISTRICT
RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA



## KUPOTELEWA KWA VYETI



**ZUHURA RAMADHANI MSOFFE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3873-0062** kilichotolewa na **UPARO SEKONDARI** mwaka 2012. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0485-1267** kilichotolewa na MAJENGO SEKONDARI mwaka 2017. Cheti cha Ualimu chenye namba **MNMA/BD.EGK/0683** kilichotolewa na THE MWALIMU NYERERE MEMORIAL ACADEMY mwaka 2020. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/177107/2024.**

HABARI KIMATAIFA

# Walz akubali ugombea mwenza Marekani

**CHICAGO, Marekani**

MKUTANO mkuu wa chama cha Democratic nchini Marekani, umemthibitisha Tim Walz, kuwa mgombea mteule wa makamu wa rais.

Walz (60) aliteuliwa na Kamala Harris (59), kuwa mgombea mwenza wake katika uchaguzi mkuu utakaofanyika Novemba mwaka huu.

Harris ambaye ni makamu wa rais aliingia kwenye kinyang'anyiro cha kuwania nafasi hiyo ya juu katika taifa la Marekani, baada ya Rais Joe Biden kujiondoa kama mgombea wa chama hicho.

Walz, anajulikana kuwa na ulimi mwepesi ambao mara alipokubali uteuzi huo, alianza kuwashambulia Trump na mgombea mwenza wake JD Vance katika hotuba yake ya kushukuru.

Mgombea mwenza huyo amesifiwa na Wademocrat kwa kumuunga mkono Harris na wanawake wengine.

Walz ameleta uhai kwenye kampeni za Harris, akijielezea yeye na Harris kama wapambanaji machachari wanaolenga kuweka mustakabali bora wa Marekani na kumtuhumu mgombea wa Republican kuzusha hofu na mgawanyiko nchini humo.

Wakati huo huo, Chanzo kimoja kimeliambia shirika la habari la Reuters kuwa mgombea huru, Robert F. Kennedy, anatarajia kufikia makubaliano ya kuungana na Trump kwa sharti la kupewa nafasi katika serikali mpya itakayoundwa.

Uungwaji mkono wa Kennedy unaweza kumsaidia Trump baada ya utafiti wa kura za maoni kuonesha uchaguzi huo huenda ukashuhudia mchuano mkali.

Trump alikutana na Kennedy mwezi uliopita kujadili uwezekano wa kupata uungwaji mkono wa wake.

Kura za maoni zinaonesha Harris akiwa mbele ya mpinzani wake huyo katika majimbo kadhaa ambayo yataamua matokeo ya uchaguzi.

***DW***



Rais wa zamani wa Marekani Barack Obama na mkewe Michelle Obama, wakiwasalimia watu walipohudhuria mkutano mkuu wa chama cha Democratic uliofanyika Chicago juzi. **PICHA: NPI**

# Mpox yaongeza hofu Afrika

**NAIROBI, Kenya**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia wahamiaji (IOM), limetoa wito wa kupatikana kiasi cha dola za Marekani, milioni 15.5 (sawa na shilingi bilioni 49.9). kwa ajili ya kupambana na ugonjwa Mpox kwa wakimbizi na jamii zinazohifadhiwa barani Afrika.

Fedha hizo zinakusudiwa kuwasaidia wahamiaji na wakimbizi katika eneo la Afrika mashariki, pembe ya Afrika na kusini mwa Afrika.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Amy Pope, alisema ugonjwa huo umeendelea kuziathiri jamii zilizoko kwenye mataifa hayo na kwamba kasi ya kuenea kwake, inaongeze haja ya kupatikana kwa msaada wa haraka.

Hadi kufikia sasa nchi ya jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo,pekee imerekodi uwepo wa wagonjwa zaidi ya elfu 10 na vifo 537, huku mataifa mengine ya Rwanda, Kenya, Uganda na Afrika Kusini yakithibitisha kuwepo kwa wagonjwa.

Wakati huo huo, Shirika la Afya Duniani (WHO) lilitoa wasiwasi kwa watu kwa kueleza aina mpya ya virusi vya Mpox sio kama COVID.

Mkurugenzi wa WHO kanda ya Ulaya, hans Kluge, alisema wataalamu wanajua jinsi ya kudhibiti kuenea kwake, hivyo watu wasifananishe na Covid-19..

"Tunaweza na lazima tukabiliane na mpox pamoja," alisema Kluge, katika mkutano na vyombo vya habari vya Umoja wa Mataifa.

"Tutachagua kuweka mifumo ili kudhibiti na kuondokana na mpox duniani kote? Au tutaingia kwenye mzunguko mwingine wa hofu na kupuuza? Jinsi tunavyojibu sasa na miaka ijayo itakuwa mtihani mkubwa kwa Ulaya na dunia, „aliongeza.

Mtu akiambukizwa Mpox, hupata vidonda vilivyojaa usaha na dalili zinazofanana na mafua ambayo huwa hafifu lakini yanaweza kuua.

Aina mpya ya virusi vya clade 1b imesababisha wasiwasi wa kimataifa kwa sababu inaonekana kuenea kwa urahisi zaidi.

Maambukizi ya aina hiyo ilithibitishwa wiki iliyopita nchini Uswis na kuhusishwa na mlipuko wa ugonjwa huo unaoendelea barani Afrika.

***TRT***

# M23 wakaribia mji wa Goma

**GOMA, DRC**

MAPIGANO mapya yameripotiwa kutokea katika Wilaya ya Masisi na kuhusisha waasi wa M 23 wanaoungwa mkono na Rwanda na wanamgambo Wazalendo wanaosaidiwa na Jeshi la Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Taarifa kutoka eneo hilo zilisema mapigano hayo yalianza usiku wa kuamkia Jumatano, yamesbabisha vifo vya raia kwenye kijiji cha Lukofu, umbali wa Kilomita 60 kutoka Magharibi mwa mji wa Goma.

Mapigano hayo makali kati ya makundi hayo mawili yakishuhudiwa kwenye eneo la Mema.

Watu watatu waliripotiwa kupoteza maisha, kwenye makabiliano hayo, huku wengine 15 wakijeruhiwa.

Mpaka sasa ni vigumu kufahamu ni nani kati ya waasi wa M23, jeshi la DRC na waasi wa Wazalendo, anayedhibiti eneo la Lukofu, huku mapigano mengine yakiripotiwa pia kwenye maeneo ya Tunda.

Aidha, waasi wa M23 wameripotiwa kudhibiti mji wa Kikovu, katika wilaya ya Lubero.

***RFI***

## Ndege mpya ya rais yaibua hasira Nigeria

**ABUJA, Nigeria**

RAIA wa Nigeria wamekasirishwa na hatua ya serikali kununua ndege mpya kwa ajili ya matumizi ya kiongozi wa nchi hiyo Bola Tinubu.

Taifa hilo la Afrika Magharibi limekumbwa na maandamano ya raia wanaopinga kupanda kwa bei ya bidhaa, ukosefu wa kazi na kushuka kwa uchumi.

Ndege hiyo Airbus A330, ilinunuliwa wiki mbili, lakini gharama yake haijawekwa wazi.

Hata hivyo, Rais Tinubu alianza kuitumia ndege hiyo mpya Jumatatu kwa kusafiria kuelekea Ufaransa. Mpaka sasa taifa hilo lina ndege tano kwa ajili ya rais pekee.

RaisTinubu ambaye alichaguliwa mwaka jana kuongoza nchi hiyo yenye watu wengi zaidi barani Afrika, alianzisha mageuzi kadhaa ya kiuchumi, ikiwa ni pamoja na kuondolewa kwa ruzuku ya mafuta, ambayo imechangia kuongezeka mfumuko wa bei, ambao umefikia zaidi ya asilimia 30.

Rais Tinubu alisema mageuzi hayo ni muhimu ili kupunguza matumizi ya serikali na kuchochea ukuaji wa uchumi.

Kiongozi huyo alitangaza kupunguza kwa asilimia 60 ya idadi ya maofisa wa serikali wanaosafiri nje ya nchi, ikiwa pamoja na wasaidizi wake mwenyewe.

***BBC***

**Hata hivyo, Rais Tinubu alianza kuitumia ndege hiyo mpya Jumatatu kwa kusafiria kuelekea Ufaransa. Mpaka sasa taifa hilo lina ndege tano kwa ajili ya rais pekee.**

HABARI MICHEZO

# AZAM YAAHIDI KUENDELEZA UBABE MASHINDANO AFRIKA

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Yossoupha Dabo, amesema amekiandaa vyema kikosi chake ili kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mechi ya marudiano ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji APR itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Amahoro jijini, Kigali.

Katika mechi ya kwanza iliyochezwa wikendi iliyopita, Azam FC ilipata ushindi wa bao 1-0.

Dabo aliliambia gazeti hili amewaandaa wachezaji wake kisaikolojia kuhakikisha wanaenda kujituma katika mechi hiyo ya marudiano kwa sababu wanataka kusonga mbele kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Kocha huyo alisema amewaandaa wachezaji wake wasahau matokeo ya mechi ya kwanza na kuingia uwanjani kwa ajili ya kupambana kusaka ushindi.

Alisema anaamini mechi hiyo ya marudiano haitakuwa rahisi kwa sababu wapinzani wao watakuwa nyumbani ambapo pia wanahitaji matokeo mazuri yatakayowapeleka mbele.

"Tunaendelea na maandalizi, tunajua mechi hiyo inatarajiwa kuwa ngumu ingawa sisi tutaingia tukiwa na faida ya ushindi wa bao 1-0, hata hivyo hatutabweteka, tutajiimarisha na kufanyia kazi mapungufu yetu.

Hatutabweta, tumejipanga kufanya vizuri katika mashindano haya msimu huu, tunawaomba Watanzania waendelee kutuombea, hatutawaangusha," alisema Dabo.

Alisema kila mchezaji ana morali ya kusaka ushindi na benchi la ufundi linaendelea kurekebisha makosa iliyobaini katika muda uliobakia.

"Nimekuwa na mazungumzo na wachezaji wangu kwa ajili ya kuwapa maelekezo ambayo wakiyafuata, nina hakika tutapata ushindi na kufikia malengo, lakini tutacheza kwa tahadhari wakati wote," kocha huyo alisema.

Azam iliyomaliza katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita pamoja na mabingwa, Yanga wanashiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Simba na Coastal Union zenyewe zinapeperusha bendera ya Bara kwenye michuano hiyo ya kimataifa.



Waamuzi wa FIFA na Elite wakiwa katika semina ya mafunzo inayoendelea kwenye Kituo cha Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kilichoko Kigamboni, Dar es Salaam kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya ulioanza wiki iliyopita hapa nchini. **PICHA: TFF**

# Singida BS yaweka kambi Dar

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Singida Black Stars kimeweka kambi jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kufanya mazoezi kwenye viwanja vya nyasi bandia kabla ya kuivaa Kagera Sugar, Jumamosi ijayo kwenye Uwanja wa Kaitaba ulioko Bukoba, mkoani Kagera.

Ofisa Habari wa Kagera Sugar, Hussein Massanza, amesema jana wamewasili Dar kwa lengo la kuweka mikakakati ya kuhakikisha wanapata pointi tatu muhimu za mchezo huo.

"Tumekuja KMC kufanya mazoezi kwa sababu tunakwenda kucheza dhidi ya Kagera Sugar ambako kuna uwanja wa nyasi bandia. Singida hakuna kiwanja chenye nyasi bandia, Uwanja wa Kaitaba una kapeti, tupo hapa kwenye Uwanja wa KMC, ambao ni wa nyasi bandia, moja wa viwanja bora, na bado ni mpya, " alisema Massanza.

Naye Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Denis Kitambi, alisema wanafanya maandalizi 'kabambe' kwa sababu wanataka ushindi na si matokeo mengine tofauti.

Kitambi alisema malengo ya timu hiyo ni kumaliza katika nafasi nne za juu msimu huu wa 2024/2025.

"Nia yetu msimu huu ipo wazi, tunataka kumaliza katika nafasi nne za juu, unajua kila baada ya mchezo tunafanya tathmini, ndiyo tumeshinda mabao 3-1 mchezo uliopita, lakini kuna maeneo tumeyaona yana mapungufu tunahitaji kuboresha, na moja ambalo tunataka kulifanya ni kutoruhusu mabao mepesi," Kitambi aliongeza.

Alisema anahitaji kukamilisha 'biashara' mapema ili kujiondoa kwenye 'presha' wakati wa lala salama.

## Simba Queens, PVB Buyenzi uso kwa uso

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha Simba Queens kinatarajia kukutana na PVB Buyenzi kutoka Burundi katika mechi ya mwisho ya Kundi B ya mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Abebe Bikila jijini Addis Ababa, Ethiopia.

Tayari Simba Queens ambayo ni vinara wa Kundi B wameshatinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo hivyo wanataka kujua timu itakayoungana na wawakilishi hao wa Tanzania.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Juma Mgunda, amesema anawapongeza wachezaji wake kwa kuendelea kujituma katika kila mechi na anaamini leo wataendelea kusaka matokeo bora.

"Nina furaha na kuona wachezaji wangu wanaendelea kupambana katika kila mechi, hakuna mechi rahisi, wachezaji wanajituma na wanataka kufikia malengo yetu na ya nchi," alisema Mgunda.

Wenyeji CBE pia wameshafuzu hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo ambayo itachezwa Jumanne wakati fainali itafanyika Agosti 29, mwaka huu

## Mingange aibukia Stand United FC

**Na Adam Fungamwango**

ALIYEKUWA kocha wa Ndanda FC na Mashujaa, Meja Mstaafu Abdul Mingange, ametua katika timu ya Stand United ya Shinyanga ambayo itashiriki Ligi ya Champinship msimu mpya.

Taarifa iliyotolewa na Stand United, inasema wamempa Mingange mkataba wa mwaka mmoja na wanaamini anauwezo wa kusaidia kuipandisha daraja timu hiyo iliyoteremka msimu wa 2018/19.

"Mingange ndiyo kocha wetu mpya, amesaini mkataba wa mwaka mmoja kuitumikia timu yetu," ilisema sehemu ya taarifa ya klabu hiyo.

Mbali na kocha huyo, Stand United imemtangaza Daudi Macha kuwa kocha msaidizi, Ally Shomari (kocha wa makipa), na kipa wa zamani wa Moro United, JKT Ruvu, Ndanda, Coastal Union, Azam na Yanga, Jackson Chove, kuwa meneja wa timu.

Tayari Stand United imewasajili wachezaji kwa wapya kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi ambao ni pamoja na John Mwanda, Ally Hamisi, Mudrick Salim na Frank Sekule.

## ZISIKUPITE

### CHILWELL ATAKIWA MAN UNITED

KLABU ya Manchester United imepewa nafasi ya kumsajili beki wa England na klabu ya Chelsea, Ben Chilwell baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kuambiwa hayupo katika mipango ya kocha, Enzo Maresca. ***(Sportsport)***

### WEST HAM KUMSAJILI SOKER

WEST Ham inataka kumsajili kiungo wa kati wa Hispania, Carlos Soler mwenye umri wa miaka 27 kutoka Paris St-Germain lakini lazima wauze wachezaji kabla ya kununua. ***(Guardian)***

### BARCO KWA MKOPO SEVILLA

MLINZI wa Brighton, Valentin Barco mwenye umri wa miaka 20 anatazamiwa kujiunga na Sevilla kwa mkopo lakini mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina haujumuishi chaguo la kumnunua. ***(Fabrizio Romano)***

### NAPOLI YASAKA NYOTA ENGLAND

MKURUGENZI wa Napoli, Giovanni Manna amerejea England kuendelea na mazungumzo ya uhamisho wa kiungo wa kati wa Brighton na Scotland, Billy Gilmour mwenye umri wa miaka 23, mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 31, na kiungo wa kati wa Manchester United na Scotland, Scott McTominay mwenye miaka 27. ***(Gianluca di Marzio)***

### MKOPO WA JEBBISON WAKUBALIWA

KLABU ya Watford imekubali mkataba wa mkopo wa msimu mzima na Bournemouth kwa ajili ya mshambuliaji, Daniel Jebbison mwenye umri wa miaka 21, mzaliwa wa Canada. ***(Sky Sports)***

### WORRALL HUYO NOTTIGHMA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest imekubali ombi la kumnunua mlinzi wa England, Joe Worrall mwenye umri wa miaka 27 kutoka Burnley. ***(Football Insider)***

### STERLING ANATAKA KUBAKI EPL

MSHAMBULIAJI wa zamani wa England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 29 anataka kubakia kwenye Ligi Kuu ya England baada ya kuambiwa hana mustakabali wa kuwa Chelsea. ***(Sky Sports)***

### CHIESA ATAKIWA BARCELONA

BARCELONA wanafikiria kumnunua mshambuliaji wa Juventus na Italia, Federico Chiesa mwenye umri wa miaka 26. ***(ESPN)***

### UGARTE WA PSG ANUKIA UNITED

KLABU ya Manchester United inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili kiungo wa kati wa Uruguay, Manuel Ugarte mwenye umri wa miaka 23, kutoka Paris St-Germain. ***(Sky Germany)***

### PATINO AKARIBIA D' LA CORUNA

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Charlie Patino mwenye umri wa miaka 20, anakaribia kujiunga na Deportivo La Coruna katika uhamisho wa kudumu. ***(Athletic)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NKETIAH AKARIBIA KUTUA NOTTINGHAM

Klabu yake inakaribia kuafikiana na wanunuzi hao baada ya awali kukataa ofa yao ya ....

**LONDON, England**

ARSENAL inakaribia kuafikiana na Nottingham Forest kuhusu Eddie Nketiah, huku ofa moja ya kumnunua mshambuliaji huyo ikikataliwa na Washikabunduki hao.

Licha ya kusaini mkataba mpya wa muda mrefu mwaka 2022, Nketiah amesalia kuwa mchezaji asiye na nafasi katika klabu ya Arsenal.

Alianza mechi 10 pekee za Ligi Kuu msimu wa 2023/24, hakupata nafasi ya kucheza hata mchezo mmoja baada ya msimu huo na alikuwa mchezaji mdogo ambaye hajatumika katika mechi ya ufunguzi ya msimu huu wa 2024/25 wikendi iliyopita.

Akiwa na umri wa miaka 25, Nketiah si kipaji kipya tena na inaonekana hana chaguo ila kuhama ikiwa anataka kucheza.

Gazeti la Athletic limeripoti kuwa mazungumzo kati ya Arsenal na Forest yanaendelea baada ya kitita cha pauni milioni 25 kukataliwa.

Washikabunduki hao wanatarajia kupata kiasi cha pauni milioni 30 au 35 kwa Nketiah, huku mazungumzo kati ya Forest na kambi ya mchezaji huyo kuhusu masuala binafsi pia yakiendelea.

Nketiah alionekana kana kwamba angejiunga na Marseille mwanzoni mwa msimu wa majira ya joto, lakini mpango huo ulivunjika kutokana na kushindwa kukubaliana kati ya klabu hizo kwenye ada ya uhamisho.

Forest walikuwa miongoni mwa timu nne pekee za Ligi Kuu msimu uliopita ambazo hazikufikisha mabao 50 katika kampeni ya michezo 38, huku kukosekana kwa umakini wa mbele kulifichuliwa na kukosekana kwa Taiwo Awoniyi.

Mkongwe wa kimataifa wa New Zealand, Chris Wood alianza na kufunga katika sare ya 1-1 Jumamosi dhidi ya Bournemouth na kufungua msimu mpya, huku Awoniyi akitokea benchi baadaye.

Nketiah hajawahi kupata nafasi ya kuanza hadi sasa, ingawa yeye ndiye mfungaji bora wa muda wote wa England katika timu ya taifa ya chini ya umri wa miaka 21.

Licha ya kuhusishwa na chaguzi kadhaa na bila shaka kuwa ndio sehemu pekee inayokosekana, Arsenal haijasajili mshambuliaji wa kati msimu huu wa joto.

Kai Havertz alijipanga kama 'namba tisa' dhidi ya Wolves wikendi na alifanikiwa, baada ya kufurahia mwisho mzuri wa msimu uliopita pia.

# MARESCA ATEMA CHECHE CHELSEA



**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Enzo Maresca amesisitiza kuwa klabu hiyo sio sehemu ya "fujo" licha ya kuwa na zaidi ya wachezaji 40 wa kikosi cha kwanza kwenye vitabu vyao huku pia akipinga madai ya Raheem Sterling kwamba yuko gizani kuhusu mustakabali wake.

Dirisha la usajili wa majira ya joto kwa Chelsea liliendelea siku ya Jumatano huku Conor Gallagher akikamilisha uhamisho wake wa pauni milioni 34 kwenda Atlético Madrid na João Félix akiwa mchezaji wa 11 kusajiliwa na klabu hiyo katika dirisha la majira haya ya joto

Maresca alithibitisha kwamba idadi kubwa ya wachezaji wanafanya mazoezi mbali na kundi la kwanza ambalo limeonekana kuwa la ziada kwa mahitaji na wachezaji kadhaa wa hadhi ya juu katika kundi hilo akiwemo Gallagher kabla ya kuondoka kwake, Ben Chilwell, Trevoh Chalobah na Sterling.

Maresca alisema: "Sifanyi kazi na wachezaji 42. Hilo ni jambo kutoka nje. Ninafanya kazi wakati huu na wachezaji 21.

"Kikao cha leo (juzi) ni cha wachezaji 20, kikao cha juzi kilikuwa na 21. Kwa hivyo wengine 15 au 20, wanafanya mazoezi tofauti ulikuwa na wachezaji 26 au 27 kwa hivyo wapo wachezaji wa Chelsea, 42, 43, ndio kwa hakika, lakini hawafanyi kazi na mimi, kila siku siwaoni kwa hivyo sio fujo kama inavyoonekana kutoka nje.

Chelsea wamepitisha sera ya kusajili wachezaji kwa mikataba ya muda mrefu, mara nyingi mikataba ya miaka minane au tisa lakini Maresca alidai sera yake ya uteuzi haitaathiriwa kama matokeo.

"Niko hapa kuchukua uamuzi na kufikiria vitu bora tu kwa ajili yetu," aliendelea. "Sifikirii kuhusu mkataba wa miaka mingapi wanao, sio kazi yangu. Kama wana mkataba wa miaka sita lakini siwapendi, wanaweza kuwa na mkataba wa miaka 20.

"Nipo hapa kufanya uamuzi sahihi kwa timu, si zaidi ya hapo. Kuhusu hali ya mkataba, sio kazi yangu."

Sterling amebakiza miaka mitatu kwenye mkataba wake Chelsea na alitoa taarifa ya kutaka kujua mustakabali wake baada ya kuachwa kwenye mechi ya ufunguzi ya Ligi Kuu ya England Jumapili dhidi ya Manchester City.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 alikuwa sehemu ya mechi zote sita za kujiandaa na msimu kabla ya kuachwa, lakini Maresca alisema: "Nilizungumza na Raheem moja kwa moja siku moja kabla ya mchezo na City na nilimweleza hali halisi.

"Sioni Raheem baada ya mchezo, anafanya mazoezi tofauti kama nilivyosema. Ikitokea nikikaa na Raheem, nitamwambia yale yale niliyokwishamwambia. Sina jipya la kumwambia. kwa sababu nilikuwa wazi kabisa."

Sterling anaaminika kufanyia kazi mustakabali wake siku zijazo, huku Juventus wakiwa miongoni mwa klabu zinazotaka kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa England kwa mujibu wa vyanzo.

Maresca pia alisisitiza kuondoka kwa Gallagher kunatokana na hitaji la kufuata kanuni za faida na uendelevu za Ligi Kuu, ambazo zinasema kwamba fedha zinazopatikana kupitia kuuza wachezaji waliotengenezwa katika akademi ya klabu zinaweza kuhesabiwa kuwa faida halisi.

## Joao Felix asaini miaka saba

**MADRID,** Hispania

CHELSEA imetangaza kumsajili Joao Felix kutoka Atletico Madrid, huku Mreno huyo akisaini mkataba wa miaka saba.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 24 alitumia kipindi cha pili cha msimu wa 2022/23 kwa mkopo na 'The Blues', akifunga mabao manne katika mechi 20 za mashindano yote kabla ya kujiunga na Barcelona kwa mkataba mwingine wa muda katika kampeni iliyofuata.

Anaungana na Omari Kellyman, Tosin Adarabioyo, Marc Guiu, Kiernan Dewsbury-Hall, Renato Viega, Caleb Wiley na Pedro Neto kama wachezaji wapya waliowasili Stamford Bridge msimu huu wa majira ya joto.

Ripoti ya Athletic imedai ada yake ina thamani ya takribani pauni milioni 44.5, huku klabu hiyo wakipata kipengele cha kuuza.

Aliiambia tovuti ya Chelsea: "Nina furaha sana kurejea Chelsea na siwezi kusubiri kuanza. Ninaweza kuona baadhi ya watu ninaowafahamu mara ya mwisho nilipokuwa hapa, ambayo ni nzuri kila mara.

Felix alisajiliwa na Atletico mwaka wa 2019 kwa kitita cha euro milioni 126 ada ya nne kwa juu zaidi kuwahi kutokea - lakini hakukaribia kulipa gharama hiyo kwa mabao 34 pekee katika mechi 131.

Alifunga mabao kumi kwa Barca msimu uliopita, baada ya kutofautiana na kocha, Diego Simeone.

Aston Villa hapo awali walikuwa wakitaka kupata Saini yake, huku kocha, Unai Emery akivutiwa na mwanasoka huyo wa zamani wa Benfica.

Kurejea kwake London Magharibi ndio biashara ya hivi punde zaidi kati ya Chelsea na Atletico, huku Conor Gallagher akihamia Hispania pia kuthibitishwa Jumatano.

Felix ni chaguo jingine la ubunifu kwa kocha Enzo Maresca katika nafasi ya tatu ya mwisho.

Christopher Nkunku na Cole Palmer walianza kwenye winga kwenye mechi ya ufunguzi ya Ligi Kuu ya Chelsea dhidi ya Manchester City, huku Enzo Fernandez akicheza katika nafasi ya namba 10 nyuma ya mshambuliaji Nicolas Jackson.

## Fernandes anafichua siri ya kukubali kubaki Man Utd

**MANCHESTER,** England

BRUNO Fernandes amefichua kuwa alitaka Manchester United kufanya maboresho makubwa kwenye kikosi chao cha kucheza kabla ya kusaini mkataba mpya.

Manung'uniko ya kutoridhika yalitoka kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno mwishoni mwa msimu uliopita alipokiri kuwa anaweza kuwahama Mashetani Wekundu ikiwa wangetaka kujijenga upya bila yeye.

Hata hivyo, kiungo huyo mshambuliaji amesaini mkataba mpya wa miaka mitatu Old Trafford.

Wamiliki wenza wapya INEOS wamekuwa na shughuli nyingi wakati wa dirisha la usajili la majira ya kiangazi, wakiwaleta Joshua Zirkzee, Leny Yoro, Matthijs de Ligt na Noussair Mazraoui, na Fernandes amekiri kuwa ana furaha kuona United ikifanya maendeleo ya wazi nje ya uwanja.

Aliambia tovuti ya klabu: "Klabu ilijua kwamba ninataka kushindana na timu bora. Walijua kwamba tulihitaji kuboresha timu. Na nadhani tunafanya hivyo.

"Ni wazi, niliwaambia, "Sihitaji uniahidi kwamba tutashinda ligi". Kwa sababu hakuna mtu anayeweza kuahidi hilo. Lakini angalau tutakuwa na timu ya kushindana na kuwa washindani katika msimu, kujaribu kupata fedha na kushindana katika viwango vya juu zaidi.

"Nadhani klabu inafanya hivyo. Inajaribu kuleta watu ili kupata wachezaji wengi wenye ubora katika timu, ili kupata ushindani zaidi, hivyo kila mtu anapigania nafasi yake.

"Lakini chaguo langu la kwanza lilikuwa kila mara kubaki kwenye klabu. Hayakuwa matakwa, lakini mambo ambayo nilitaka kuona, klabu kwenda mbele. Kusema kweli, naangalia sasa na naona klabu inafanya juhudi katika hilo."

Fernandes alianza mechi ya kwanza ya Ligi Kuu ya United Ijumaa iliyopita huku Zirkzee akifunga bao la ushindi dakika za lala salama katika ushindi wa 1-0 dhidi ya Fulham.

HABARI MICHEZO

# YANGA KUSAJILI WACHEZAJI WAGENI WAWILI DESEMBA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Yanga ikijiandaa na mchezo wake wa marudiano ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Vital'O kutoka Burundi, Rais wa klabu hiyo, Hersi Said, amesema wanatarajia kusajili nyota wapya wawili katika dirisha dogo la usajili litakapofunguliwa baadaye mwaka huu.

Hersi alisema hayo jijini jana na kuongeza kuwa nyota hao watakaosajiliwa watakuwa ni wachezaji wa kigeni.

Alisema licha ya kikosi cha Yanga kuonekana ni ‚tishio', lakini viongozi wanaona hakijakamilika katika kiwango wanachohitaji kifike.

"Kikosi hiki hakijakamilika, bado, nataka niwaambie tu, Yanga hii bado, tena kuna mchezaji tulitakiwa tumlete kwenye hili dirisha kubwa lakini dili halikukamilika, na baada ya hapa, Januari kutakuwa na ongezeko la wachezaji wengine wawili wa kigeni. Kwa hiyo haijakamilika, ikikamilika ndiyo wanahabari tuulizeni kuhusu ubingwa wa Afrika, lakini kwa sasa bado," alisema Hersi.

Aliongeza lengo ya Yanga kwa sasa ni kufika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na si vinginevyo.

"Sisi malengo yetu ni kufika robo fainali, tunataka tuingie makundi tuzoee kwanza makundi, halafu twende robo fainali, ila wakati mwingine Mungu huwa ana zawadi, akitupa nusu fainali, fainali au tukichukua ubingwa, sawa tunashukuru, lakini lengo ‚mama' ni robo fainali," Hersi alisema.

Wakati huo huo, mchezo wa marudiano kati ya Yanga na Vita'O sasa utachezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam badala ya Azam Complex, imeelezwa.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo, imesema mchezo utachezwa Jumamosi kuanzia saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania kama ilivyopangwa awali.

Yanga itashuka dimbani ikiwa na faida ya ushindi wa mabao 4-0, walioupata kwenye mechi iliyopita.




Naibu Waziri Sanaa, Utamaduni na Michezo, Hamis Mwinjuma ‚Mwana FA' akitumbuiza wakati wa Usiku wa Singeli wa NMB katika Tamasha la Kizimkazi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwana FA apagawisha Usiku wa Singeli NMB Day

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Khamis Mwinjuma "Mwana FA", amepagawisha mashabiki waliohudhuria Usiku wa Singeli wa Siku ya Benki ya NMB 'NMB Day' katika Tamasha la Kizimkazi, ambako alitumbuiza kwa dakika 10.

Usiku wa Singeli ulikuwa hitimisho la NMB Day, siku maalum iliyotumika kukabidhi na kuzindua miradi iliyotekelezwa na NMB katika Kizimkazi Festival, ambako ilikabidhi Skuli ya Maandalizi kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na kung'arishwa na bonanza la michezo.

Mgeni rasmi wa Usiku wa Singeli alikuwa ni Waziri wa Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Tabia Maulid Mwita.

Mwana FA, nyota Hip Hop wa lililokuwa Kundi la East Coast Team, alipanda jukwaani saa 3:45 usiku, ambapo alianza kutoa hotuba fupi kabla ya mashabiki kumshawishi atumbuize, ndipo alipoanza michano ya kibao chake cha Habari Ndio Hiyo, Unanijua Unanisikia.

Baada ya mistari michache ya Unanijua Unanisikia, MwanaFA akadondosha 'vesi' moja ya kibao chake kiitwacho Mfalme alichomshirikisha G Nako, kabla ya kugeukia singeli na kuchana 'free style' kali na kumalizia kibao cha Sio kwa Ubaya alichoimba na Harmonize.

"Nimshukuru Waziri Tabia kunichagua kuambatana nami hapa, niwashukuru marais wetu Dk. Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa kazi kubwa wanayofanya kuipambania sanaa ya Tanzania, ambayo inapaswa kupambaniwa pia na wasanii wenyewe," alisema Mwana FA.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwan Kikwete, ndiye aliyekabidhi vikombe kwa washindi wa bonanza hilo lililohusisha michezo ya karate, bao la kete, karata, kufua na kukuna nazi na kuvuta kamba.

## Rais Samia azishushia neema Simba, Yanga

INATOKA UK. 24

AFCON ambapo Tanzania inatarajia kuwa mwenyeji wa mwanza wa fainali za mwaka 2027 pamoja na nchi za Kenya na Uganda.

Aidha aliagiza kuendelea na kasi ya ujenzi wa viwanja ili vikamilike kwa wakati kwa ajili ya fainali hizo vikiwemo viwanja vinavyojengwa Arusha, Dodoma pamoja na Dar-es-Salaam.

Akizungumzia ujenzi wa kituo cha michezo Kizimkazi, aliwataka vijana kuchangamkia fursa za kuwepo kwa kituo hicho ambacho walengwa wake wakubwa ni kundi la vijana pamoja na watoto katika kukuza na kuibua vipaji vya michezo.

Alisema Vijana wanahitaji kuandaliwa mapema katika masuala mbali mbali ya msingi ikiwemo michezo hatua ambayo itawawezesha kuibuliwa kwa vipaji vyao na baadaye kuwa nyota wa michezo mbali mbali na kufikia kiwango cha kujiajiri.

‚'Akademi hii walengwa wake wakubwa ni kundi la vijana na watoto ambao vipaji vyao vitaibuliwa na kuweza kuvitumia katika maeneo mbali mbali na kuweza kujiajiri katika michezo"alisema..

Rais Samia, alisema wananchi wa Kizimkazi na Zanzibar kwa ujumla sasa wapo tayari kwa ajili ya ujenzi wa Akademi hiyo ya michezo ambapo wamechangia jumla ya Shilingi Bilioni mbili mradi huo ukamilike mwaka 2025 kama ilivyopangwa.

"Abebwaye hujikaza sisi wananchi wa Kizimkazi wilaya ya Kusini katika kuonesha utayari wetu wa ujenzi wa kituo cha michezo cha Suluhu Akademi tunachangia Shilingi bilioni mbili ili kuongeza ari kwa kushirikiana na wafadhili wetu", alisema Rais Samia.

Akizungumza kwa upande wake, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema Rais Samia amekuwa mdau mkubwa wa michezo mbali mbali kwa kuongeza hamasa kwa vilabu vya soka ikiwemo Simba na Yanga kuona vinapata ushindi mkubwa katika mashindano ya kimataifa.

Aidha alizitaja juhudi zinazochukuliwa na Rais Samia katika michezo ni pamoja na kuona ujenzi wa viwanja vya kisasa unafanyika nchini, hatua ambayo ni sehemu ya kuitangaza nchi katika ushindani wa soka na michezo mingine.

Aidha, mfadhili mnkuu wa mradi wa ujenzi wa kituo cha michezo chja Suluhu, benki ya CRDB kupitia Mkurugenzi Mtendaji wake, Abdulamajid Nsekela, alisema maandalizi ya ujenzi wa kiwanja cha kisasa cha Suluhu Akademi yameanza huku ujenzi huo ukitoa ajira kwa makundi mbali mbali ya wananchi wa kijiji cha Kizimkazi.

Nsekela alisema kituo hicho kikikamilika kitakuwa na uwezo wa kuchukua vijana 170 na kuwapatia mafunzo na kuwaandaa katika maeneo mbali mbali ya michezo.

Michezo
Ijumaa Agosti 23, 2024
Nipashe

**Nketiah akaribia kutua Nottingham Forest**

UKURASA 21





# Rais Samia azishushia neema Simba, Yanga

●●●Asema yeye yupo katikati ya klabu hizo na amezitafutia wadhamini wapya ili kuzisaidia kuweza....

**Faustine Feliciane na Rahma Suleiman**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema amefanya mazungumzo na wadau na wawekezaji wakubwa hapa nchini kwa ajili ya kuzidhamini klabu za Simba na Yanga ili ziendelee kufanya vizuri.

Akizungumza jana kwenye uwekaji wa jiwe la msingi kwenye ujenzi wa kituo cha michezo na ufundishaji cha Suluhu Academ, Kizimkazi, Zanzibar, Rais Samia, alisema amekuwa akizifuatilia timu hizo na siku zote yopo katikati na anafurahi pale zinapofanya vizuri.

"Najua wadhamini au washika vilabu hivi wanafanya jitihada kubwa sana, lakini pamoja nao nimeongea na wadau, wawekezaji wetu wakubwa hapa, mmoja nimempa Yanga, mmoja nimempa Simba awasaidie,“ alisema Rais Samia.

Aidha, alisema suala hilo litakapokamilika vilabu hivyo vitapewa taarifa na kuitwa kwa mazungumzo na hatua nyingine.

Katika hatua nyingine, Rais Samia, amesema kuwepo kwa viwanja vya kisasa vikiwemo vya soka kwa kiasi kikubwa kutaiwezesha Tanzania kuwepo katika ramani ya kimataifa na kuruhusu michezo mingi ya kimataifa kufanyika hapa nchini.

Alisema kuwepo kwa viwanja hivyo ni fursa ambayo itaiwezesha Tanzania kuandaa mashindano mbali mbali makubwa ya kimataifa zikiwemo fainali za Afrika,

INAENDELEA UK. 23

## Bodi ya Ligi kukusanya maoni udhamini wa klabu

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi imesema kuwa inakaribisha maoni ya wadau wote ambao wanaona hakuna haja ya mtu, kampuni au taasisi kudhamini zaidi ya timu moja kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ili iundwe kanuni rasmi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa bodi hiyo, Almasi Kasongo, amesema jana kuwa, kwa siku za karibuni kumeibuka hoja na mjadala kwa wadau wa soka ambao wanadhani kuna haja ya kuzuia mdhamini mmoja kudhamini zaidi ya timu moja, na kwa kuwa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) na Bodi ya Ligi wanaendesha soka kwa uwazi na usikivu, hawajafunga milango badala yake wanakaribisha maoni.

Hata hivyo, Kasongo, amesema maoni hayo yatatolewa kwa ajili ya kanuni ya msimu ujao, kwani msimu huu tayari wameshafunga na hakukuwa na mdau yoyote aliyelalamikia suala hilo.

„Hizi siku mbili tatu umekuwa mjadala mkubwa, lakini kwa wakati huu tuliokuwa nao hakuna kanuni inayozuia mdhamini mmoja kudhamini zaidi ya timu moja. Udhamini ni jambo la kikanuni, madhumuni ya kanuni kwa asilimia 90 yameelekezwa kwenye klabu husika, timu, wachezaji, waamuzi, viongozi, mbali na mijadala iliyoibuka, hakuna klabu yoyote au mdau kuelekea msimu huu aliyelalamikia suala hilo,“ alisema Ofisa Mtendaji huyo.

Hata hivyo, alisema kanuni siyo msahafu, hivyo kama wadau wataona kuna haja ya kuja na kanuni hizo, milango iko wazi.

„Lakini mimi siku zote nimekuwa nikiamini kuwa kanuni siyo msahafu, zinajadilika, zinabadilishika kwa hiyo pale ambapo wadau wataona kuna haja ya kufanya mabadiliko ya kanuni kama ambavyo siku zote tumekuwa tukifanya basi milango ipo wazi,“ alisema Kasongo.

Alisema wao kama viongozi wa soka, wataka kuongoza vile ambavyo wadau wa soka wataona inafaa na kuthamini michango yao. Kwa siku za karibuni kumeibuka mijadala kwa wadau wa soka vikihusu uhalali wa mdhamini mmoja kudhamini zaidi ya klabu moja kwenye ligi moja.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >